

KITENDAWILI



Tunapoendelea kusimama kwa muda kidogo tu, na tuombe.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha rehema katika Jina la Bwana Yesu. Tunakaribia mwisho wa mkutano huu sasa, nasi tumeambiwa katika Maandiko ya kwamba Yesu mwishoni mwa ile karamu, alisimama na kupaza sauti, huenda kulikuwa na matarajio ambayo Yeye alikuwa ametumaini kwamba yangetimizwa. Mungu, tunangojea kwa hamu kuu, tukijua udhaifu wa wanadamu, bali Mungu, tumetarajia kumwagwa kukuu kwa Roho Wako, kitu kisicho cha kawaida.

³ Nami ninamwangualia maskini mtumishi Wako, Carl Williams, naona maskini mikono yake iliyopinda, na akikwaruza miguu yake sakafuni, ameketi hapa akiendelea kimimina kitu fulani puani mwake apate kupumua, nikijua ya kwamba mchana na usiku amefanya kazi na kujitahidi, na moyo wangu unamwonea huruma. Mungu, Wewe hutamfisha moyo.

⁴ Na juma hili, nikipitia humu bondeni pamoja na hawa, watumishi Wako, nikihubiri makanisani mwao, kamwe hawakuniambia la kuzungumzia, walisema tu, “Endelea.” Kuona huo ushirikiano mzuri na roho ya kupendeza, wao pia, wako hapa wakingojea jambo fulani litukie, kwa hiyo tunamhisi kabisa Roho Mtakatifu akilia ndani yetu, “Njoo, Bwana Yesu.” Ijaze mioyo yetu inayotarajia, tupe kile tunachotafuta, Bwana, kipimo kikubwa cha neema Yako, tunaomba.

⁵ Hatustahili kuomba baraka kama hizo, Bwana, hakuna mmoja wetu anayestahili, lakini hatushikilii hiyo, tunawazia tu juu ya Dhabihu ambayo Yesu alitutolea apate kutusafisha. Nasi tunakuja tukiomba katika Jina Lake sasa, kwamba kila moyo utahudumiwa wakati fulani kati ya sasa na kufungwa kwa ibada, kwamba tutakapoondoka leo kutoka hapa na kwenda mahali petu mbalimbali, jalia tuweze kusema kama wale waliokuwa wakitoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?”

⁶ Kwa kuwa Bwana aliyefufuka alitembea pamoja nao, Naye akafanya jambo fulani katikati yao. Baada ya kutembea pamoja Naye siku nzima, nao hawakuelewa kabisa kwamba Yeye alikuwa ni Nani, walijua ilikuwa ni baraka kuwa pamoja na Mwalimu kama huyo. Lakini alipofanya jambo fulani kama tu alivyolifanya kabla ya kusulubiwa, walijua hakuna mtu aliyefanya *hilo* namna *hiyo* ila Yeye, nao kweli wakajua ya kwamba ilikuwa ni Bwana Yesu, upesi wakaenda kuwaambia wengine.

7 Mungu, tunaomba ya kwamba itajirudia tena leo. Tutendee mengi na kwa wingi zaidi, Bwana, huenda tukaondoka kwenye mkutano huu Jumatatu usiku, tukienda nyumbani mwetu na mahali mbalimbali, na kusema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, tulipomsikia Yeye akinena kupitia watumishi Wake kote katika huu mkutano?” Tujalie mambo haya, Bwana, kwetu sisi watumishi wasiostahili, katika Jina la Mtoto Wako Mtakatifu, Yesu. Amina.

8 Ketini. (*Huyu* ni ndugu yako wa Biblia? *Huyu*?) Huu hakika ni wakati usio wa kawaida kwangu, nami nina matumaini makubwa pia, na matarajio ya jambo fulani kutukia kwenye mkutano huu ambalo ni tofauti. Na kama tunapaswa kufunga ibada alasiri ya leo, nina hakika kwamba sisi sote tungeweza kusema, “Imekuwa vema kuwa hapa,” usiku wa kwanza kumsikia Ndugu Oral Roberts, na ujumbe wake mkuu kwa watu wa upotovu wa uadilifu wa watu, ndipo ukaja mmoja wa jumbe zenye nguvu sana za dakika kumi na mbili ama kumi na tano, kutoka kwa Ndugu yetu Velmer Gardner. Nilimtazama na kumpenda kwa upendo mkuu. Jinsi ambavyo angeweza kushindilia mengi sana katika muda mfupi tu!

9 Nilikuwa nikimwambia mke wangu, huko nyuma, kwamba, kulihusu tulipofika nyumbani, naye akasema, “Vema,” kasema, “Bill, hivyo ndivyo wao siku zo-... Wewe huwaweka muda mrefu kupita kiasi.”

10 Nikasema, “Mpenzi, mimi ni mwenda pole sana, si—siwezi kuliwazia upesi hivyo. Mungu amenirehemu tu kuniacha niwe mwenda pole, nadhani, na kwa namna fulani kuniacha niendeleo, kunionyesha wema Wake.”

11 Kisha kumsikiliza daktari wa tiba hivi majuzi usiku... (Naam, kweli ni jana usiku, Ndugu Shakarian.) Mwajua, nina marafiki wengi wazuri madaktari wa tiba. Nilihojiwa kwa Mayo, mwajua, mnalo hilo gazeti, *Ninii—Ninii*, ninaamini linaitwa *Ninii*. . . Loo, *Reader's Digest*, yapata miaka mitano iliyopita, *Muwijiza Wa Donny Morton*, kule California, Nilikutana na hilo kundi la madaktari huko, jamaa wazuri sana unaotaka kukutana nao.

12 Lakini nilipomsikia daktari yule hivi majuzi usiku, akitoa maonyo hayo kumhusu Yesu, nilifikiri huenda akawa mzuri sana katika ubainishaji wake kama—kama alikuwa anaenda kuuchunguza mwili wa kawaida. Wala hakufanya vizuri sana, ama, kazi mbaya sana katika ubainishaji wa hali ya kiroho, alikuwa na ubainishaji mzuri sana wa jambo hilo, na maneno aliyosema. Natumaini kamwe haitanibidi kuihitaji huduma yake, lakini kama nikiihitaji, ninataka mtu kama huyo kufanya huo upasuaji, kama kamwe itanibidi kufanyiwa mmoja, mtu ambaye anamtumainia Bwana.

13 Pamoja na hayo, na kuwasikia watu wengine, baadhi yao hata sikuwajua, hakika ninaamini lingekuwa jambo zuri kama tungeenda tu Nyumbani sasa hivi, lingekuwa ni jambo zuri sana. Lakini ninaamini atatujalia baraka zingine zaidi, kwa sababu kuna wengi hapa.

14 Ninangojea kumsikia huyu Ndugu Brown, ninaamini, kesho usiku. Na kamwe sijawahi... Mwepiskopalia, huh? [Ndugu fulani anasema, “Mpresbiteri.”—Mh.] Mpresbiteri. Kosa kama hilo, afadhali nisome Maandiko na kuendelea, sivyo? Hebu niseme hivi, Ndugu Brown: “Ndugu katika Kristo.” Ninajua niko sawa basi. Nimesikia mengi kumhusu, na hakika ninataka kumsikia.

15 Nitapata kukutana na marafiki zetu wote. Halafu maskini ule ujumbe mdogo uliokatikakatika, uliochochewa, jana asubuhi, kisha kumwona Shetani akimrukia maskini mwanamke mmoja, tukamtoa nje haraka, loo, laiti watu, wanalikuwa tu wa kiroho! Nikiwa nimesimama hapa, nilihisi shinkizo hilo kubwa. Alitoka nje, nami nikaomba, “Baba wa Mbinguni, mtume Roho Mtakatifu amfuate.” Akamkamata moja kwa moja *huko* nje, akamrudisha, tukamtoa huyo mwovu kutoka kwake. Nami nasikia ana Roho Mtakatifu sasa. Ninii tu, kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo. “Kwa Jina Langu watatoa pepo.”

16 Sasa, hebu na tufungue A—Andiko, nami nina yapata kurasa sita zake zilizoandikwa hapa chini, bali sitazifikia hizo zote, bali—bali chache tu. Na nitoe tu shukrani zangu kwenu nyote kwa ajili ya ushirika wenu mwema, ushirikiano, na mnaweza kunivumilia jinsi mnavyofanya.

17 Tulikuwa kwenye kanisa dogo asubuhi ya leo, Church of God, hapa, mahali fulani huku nyuma, tulipanda *hivi*, kisha tukarudi, ni—nisingejua ilikuwa ni wapi, lakini bila shaka mchungaji mzuri huko pia. Nalo kanisa hilo lilikuwa tu limengojea, nilikuwa nimechelewa tu kwa siku kumi kanisani, nikachelewa siku kumi, lakini bila shaka tulikuwa na wakati mzuri sana, tukishiriki pamoja na Bwana Yesu.

18 Sasa, ninyi mnaoandika mafungu, kama ningeyaita hivyo, ama, mwandike somo la Maandiko, kutoka kwa Yoshua, Kitabu cha Yoshua, nikihisi ya kwamba Roho Mtakatifu ameliweka hili moyoni mwangu kwa ajili ya alasiri ya leo, Yoshua 10:12, kifungu kimoja:

Ndipo Yoshua akanena na BWANA, katika siku hiyo ambayo BWANA aliwatoa Waamori mbele ya wana wa Israeli, akasema mbele ya macho ya Israeli, wewe Jua, simama kimya juu ya Gibeoni; na wewe Mwezi, simama katika bonde la Aiyaloni.

¹⁹ Mnasema, “Hilo ni somo lisilo la kawaida,” hiyo ni kweli, ama, “somo la Maandiko lisilo la kawaida.” Somo langu alasiri ya leo ni, *Kitendawili*.

²⁰ Mnajua, Mungu huchukua mambo yasiyo ya kawaida, hufanya mambo kwa njia zisizo za kawaida, na Yeye si wa kawaida kabisa, bali Yeye hufanya mambo yote pamoja kwa manufaa ya wale wampendao. Tukichukua kutoka kwenye hili, hitimisho la somo la, *Kitendawili*.

²¹ Sasa, nilienda, nikiwazia hilo, nikachukua kamusi, Nami nikawazia, “Hilo kidogo ni neno lisilo la kawaida, hatulitumii mara nyingi sana.” Ndipo nikawazia, “Labda, Bwana, kwa sababu Wewe uliweka hilo moyoni mwangu, huenda kukawa na kitu fulani hapo ambacho ninapaswa kuchuguza.” Nayoy kamusi ya Webster inasema *kitendawili* ni “jambo lisiloaminika lakini ni la kweli, jambo lisiloaminiki, bali hata hivyo ni kweli.” Halionekani kama linaweza kuwa ni kweli hata kidogo, bali ni kweli, hicho ni *kitendawili*.

²² Nikaanza kuwazia basi ni vitendawili vingapi ambavyo tungeweza kuonyesha, na kama tungesimama alasiri ya leo, ingekushangaza kuona ni mambo mangapi ambayo kisayansi yasingewezekana, lakini hata hivyo yanawezekana. Dunia hii kuning’inia angani ni kitendawili. Tunaambiwa ya kwamba inazunguka, ikifanya duara yake kamili kila saa ishirini na nne, na kuzunguka dunia ni karibu maili elfu ishirini na tano. Nanyi mwajua, mnaweza. . . Hakuna kitu ulimwenguni kitakachosonga mbele kikamilifu *hivyo* kama hiyo dunia ifanyavyo. Nako kupatwa kwa mwezi kutoka kwenye mfumo mkuu wa jua, zinasimamaje hewani, zikizunguka kikamilifu hivyo, na kuzunguka ikweta, hata unaweza kuziwekea wakati kwa muda wa miaka ishirini au thelathini, wala hazitakosea sekunde moja?

²³ Ninayo saa hapa, nami nilipewa na marafiki wazuri huko ng’ambo nilipokuwa Uswisi, saa ya kawaida tu ya Uswisi, saa ndogo ya mkono labda inagharimu kama dola mia moja na hamsini, ama kitu fulani, bali ni nzuri, kwangu mimi. Nayoy inaitwa Vulcain Cricket, na ni moja ya saa nzuri sana nilizowahi kuvaa, hata hivyo, ninaweza kuweka wakati na kuirekebisha, katika miezi miwili au mitatu ama imeenda mbio ama polepole. Wala hakuna kitu tulicho nacho kitakachodumisha chochote kikamilifu.

²⁴ Lakini wakati wa Mungu ni mkamilifu, haukosi mdundo hata mmoja. Mpira huu mkuu wa kimbinguni unaning’iniaje hewani, pasipo kufungiwa kwa chochote, ukijizungusha huku na huku namna *hii* kila saa ishirini na nne, na kila baada ya miezi kumi na miwili unazunguka kabisa, ukirudi kutoka kwenye jua? Kiangazi, baridi kali, majira ya kupukutika majani, kuchipua, kikamilifu tu, vivyo hivyo hasa, na umekuwa ukifanya hivyo

kwa maelfu ya miaka. Hakuna mtu duniani anayeweza kuelezea jambo hilo.

²⁵ Juu na chini ni wapi? Ncha ya Kaskazini iko juu, au Ncha ya Kusini ndiyo iliyo juu? Hatujui, kwa sababu tuko angani. Nawe unaweza kutupa mpira hewani na kuuangalia, hautafanya mizunguko miwili mahali pamoja. Unaanguka, unapanda juu, na unajitengenezea upepo wake wenyewe, na, kama tu vile dunia, nguvu za uvutano zinaushikilia, lakini hautapinduka mara mbili mahali pale pale, ama unapanda juu au kushuka chini. Lakini hata hivyo, mpira huu mkubwa umepinduka kwa maelfu mara maelfu ya miaka, pasipo kukosea hata kidogo. Hicho ni kitendawili.

²⁶ Ni kitendawili unapoutazama huo mwezi. Angalieni maji kujaa na kupwa huku pwani, jinsi yale mawimbi yenye hasira huku karibu sehemu nne kwa tano za dunia, zikiwa majini, nenda ufukoni mwa bahari ukaangalie hayo maji huku mawimbi hayo yenye hasira, makubwa, yakitokea huko nje, nusu maili huko nje baharini ama zaidi, yakiupigapiga ukingo huo wa bahari, kwa nini hayavuki kuja huku? Kuna kitu kimoja tu kinachoyazuia kufanya hivyo, hicho ni mwezi. Huo mwezi: Mlinzi wa Mungu, yeye hulinda ufuo huo wa bahari kwa sababu Mungu ameweka mipaka yake, wala hayawezi kuivuka hiyo.

²⁷ Lakini wakati huo mwezi unapoanza kugeuka kumwanguka Baba, angalia kwamba maji hayo yatatoka upesi, au, kuingia upesi, ndipo anapogeuka tena, yanachukua mahali pake tena. Ha—hayana budi kufanya hivyo, kwa sababu ni mlinzi wa Mungu.

²⁸ Huo mwezi, ulio umbali wa mamilioni ya maili kutoka duniani, unawezaje kuiathiri dunia? Unawezaje kuchora mstari? Kwa nini bahari hiyo isiingie maili mia chache kisha isimame? Kwa sababu Mungu aliweka mipaka yake, haiwezi kuipita hiyo, Naye ana mlinzi wa kuhakikisha kwamba haitapita.

²⁹ Na mtu yeyote anajua wakati mwezi unaposhuka, kujaa na kupwa kwa maji kunaambatana nao, ukiinuka, yanajaa pamoja nao, kitendawili kingine, hakuna mtu anayeweza kuelezea. Hatujui jinsi gani, ni matokeo gani ambayo mwezi huo juu ya nchi ungekuwa nayo, na ungefanya nini kwa kujaa na kupwa kwa maji? Mnaona? Ni kitendawili.

³⁰ Tunaweza kupanda mbegu ardhini, na mbegu hiyo itakaa ardhini kote katika majira ya baridi kali, kama vile nga—ngano, hiyo mbegu ya ngano ina ngozi upande wa nje, kisha ndani ni nyama yake, na katikati ya nyama hiyo kuna seli zazi, huo ni uhai; hivyo ndivyo ulivyoumbwa wewe.

³¹ Wewe unaninii . . . una nafsi, mwili, na roho. Upande wa nje, ambao ni mwili, unatawaliwa na hisi tano, unaingia kwenye mwili huo kwa hisi tano, kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Ndani ya huo mwili kuna nafsi, nafsi hiyo ina milango

mitano, dhamiri, na kadhalika, kumbukumbu. Lakini ndani ya hiyo kuna roho, hiyo ndiyo inayoziongoza zote, kuna mlango mmoja tu kwa hiyo, na huo ni uhuru wa kujichagulia, kutenda, kupokea, ama kukataa.

³² Nayo hiyo mbegu ikipandwa ardhini, basi inakuwaje? Majira ya baridi kali huja na kuipasua, ngozi imetoweka, nyama yake imekwisha, ndipo hiyo seli zazi ya uhai, huwezi kuipata, lakini katika majira ya kuchipua inarudi tena.

³³ Hapa siku moja nilikuwa huko chini Kentucky, nikiwinda kuchakulo. Nami . . . Sisi . . . Hali ya hewa ilikuwa ni kavu wala tusingeweza kuwapata kuchakulo wowote, kwa hiyo tukaenda kwe—kwenye sehemu ya nchi yenye korongo. Bw. Wood, rafiki yangu, akasema, “Vema, Ndugu Branham,” kasema, “Ninajua mtu huko ambaye ana miti mingi, na kuna mabonde makubwa huko chini kabisa. Labda kutakuwa na unyevunyevu, tunaweza kunyemelea humo.”

³⁴ Basi nikiwa kule, mbona, tulifika kwenye nyumba fulani, naye akasema, “Nisingetoka nje, maana jamaa huyu ni kafiri.” Kasema, “Kamwe hamwamini Mungu, naye hulaani mawazo yenyewe ya Mungu.”

Nikasema, “Vema, nitakaa kwenye gari.”

³⁵ Kwa hiyo basi, tukaenda kule, naye akaenda chini ya mtofaa ambapo huyo mzee alikuwa ameketi, yapata sabini na mitano, naye akazungumza naye, na kumwita kwa jina, akasema, “Jina langu ni Banks Wood.” Akasema, “Ningetaka kujua kama tunaweza kuwinda kwako.”

Huyo jamaa mzee akamtazama, kasema, “Wewe ni mwana wa Jim Wood?”

Akasema, “Naam.”

³⁶ Akasema, “Karibu, popote unapotaka kwenda, nafasi kubwa hapa, nina ekari mia tano za misitu.” Akasema, “Vema, Jim anaendeleaje?” Akazungumza kwa muda kidogo tu.

³⁷ Ndugu Wood akasema . . . Sasa, yeye alikuwa Shahidi wa Yehova ambaye mvulana wake, aliyelemaa, mguu mmoja umekunjamana chini yake, aliponywa mkutanoni. Yeye ni mkandarasi, kwa hiyo aliacha tu kazi ya ukandarasi, akahama akawa jirani yangu wa karibu, amekuwa huko karibu miaka kumi. Sasa, watu wake wote, kwa maono, kila mmoja wao, hata wasomaji katika shirika la Mashahidi wa Yehova, kila mmoja amejazwa na Roho Mtakatifu.

Kwa hiyo basi sisi tukisimama pale, alisema, “Nilikuja pamoja na mchungaji wangu.”

³⁸ Ndipo jamaa huyu mzee akasema, “Wood, usiniambie umekuwa duni sana, hata inakubidi kuambatana na mhubiri popote uendapo?” Ndipo nikawazia wakati ulikuwa umewadia, mimi, kutoka kwenye gari basi.

Kwa hiyo nikatoka kwenye gari, nikatembea karibu na mahali yule mzee mwungwana alipokuwa ameketi, nikasema, “U hali gani?”

Akasema, “U hali gani, bwana?” Naye akasema, “Nawe ni mhubiri ati?”

Kasema, nikasema, “Naam, bwana, ninadhaniwa kuwa.”

Naye akasema, “Vema,” akasema, “Siwazii mengi juu ya hao jamaa.”

Nami nikasema, “Vema, hao ni jamaa wazuri sana, wengi wao.”

Akasema, “Vema, hao wa namna hiyo ndio sijakutana nao bado.”

Nami nikasema, “Naam, bwana.”

Naye akasema, “Ninaamini . . .”

Nikasema, “Ni kitu gani kinachokufanya useme hivyo?”

³⁹ Akasema, “Ninaamini wanabwekea mti usiohusika.” Sasa, kila mtu anajua ya kwamba mbwa unayewinda naye usiku, naye anabwekea, mti usiohusika, unapumbazwa sikuzote. Kwa hiyo akasema, “Wanabwekea mti usiohusika.” Naye akasema, “Wanadai kuwa wamekimbiza Kitu fulani mtini, bali kamwe huwezi kukiona.”

“Naam, bwana.”

Naye akasema, “Sikuzote wanazungumza juu ya Kitu fulani, bali hawawezi kutoa chochote.”

“Naam, bwana.”

⁴⁰ Akasema, “Kulikuwa na mhubiri fulani aliyekuja hapa yapata miaka miwili iliyopita, hapa juu kwenye mahali padogo panapoitwa Acton, huko kwenye Uwanja wa Kambi wa Methodisti, walikuwa na mkutano.” Kasema, “Kulikuwa na dada mzee, anayeishi hapa juu kilimani, alikuwa akifa kwa kansa.” Kisha kasema, “Mtu huyu hakuwa amewahi kuwa humu nchini.”

⁴¹ Ndipo kasema, “Kwenye mkutano usiku ule ambapo watu elfu kadhaa walikuwa wamekusanyika,” akasema, “dada wa mwanamke huyu alikuwa ameketi mle ndani akimlilia dada yake.” Kasema, “Hata asingeweza kukalia maliwato ya kitandani tena, ilitubidi mimi na mke wangu kuvuta shuka la kuchomoa kutoka chini yake.” Kisha kasema, “Yeye . . . Dada yake huko nje pamoja na . . . akilia.” Kasema, “Mhudumu huyu alimwalia mwanamke yule, na kuliita jina lake, na kusema, ‘Unamlilia dada anayekufa kwa kansa kwenye kilima fulani.’ ‘Naam,’ akasema yule mwanamke.”

⁴² Kasema, “Huyo mhudumu akasema, ‘BWANA ASEMA HIVI: Chukua lesa hiyo sasa hivi, uliyo nayo kwenye pochi yako, uliyoweka kwenye pochi yako ulipoondoka nyumbani, na uliitoa

kwenye mtoto wa meza wa kabati la jikoni, lesu ndogo yenye herufi pembeni mwake, lesu nyeupe yenye herufi za samawati, chukua lesu hiyo na kuiweka juu ya huyo mwanamke katika Jina la Bwana.' Kisha kasema, 'Atapata afya.'"

⁴³ "Vema," kasema, "huyo mwanamke akaondoka mbio pamoja na watu wengine zaidi." Ndipo kasema, "Kusema kweli, ni karibu maili tatu, huko," kisha kasema, "tulifikiri walikuwa na Jeshi la Wokovu kando ya kilima yapata saa nne usiku mmoja." Lakini kasema, "Tulienda huko kesho yake asubuhi, naye maskini mama huyo alikuwa ameamka akipika kiamshakinywa, akila kiamshakinywa cha sambusa za matofaa yaliyokaangwa." Kisha kasema, "Hiyo imekuwa miaka miwili ama mitatu iliyopita." Kisha kasema, "Unajua, hata hajakuwa na siku aliyokuwa mgonjwa tangu wakati huo." Akasema, "Sasa, laiti ningaliweza kuona jambo kama *hilo* likitukia."

⁴⁴ "Loo," nikasema, "wewe..." Ndugu Wood akaniangalia, nami nikatikisa kichwa changu. Kwa hiyo akasema... Nimesimama pale, uchafu na damu ya kuchakulo, na kila kitu, masharubu yapata urefu *huo*, tumekuwa vilimani tukipiga kambi, ndipo ni—nikasema, "Hilo kweli linakukanganya?"

Akasema, "La, bwana."

Nikasema, "Unajali kama nikichukua moja ya hayo matofaa?"

Akasema, "Karibu, manyigu wanayala."

Nikasema, "Vema." Nikalisugulia kwenye suruali yangu chafu nikaliuama, nikasema, "Hilo ni tofaa zuri."

Akasema, "Kweli kabisa. Niliupanda mti huo pale miaka thelathini na mitano iliyopita."

"Um-hum." Nikasema, "Hebu tuone, hili ni karibu juma la mwisho la Agosti."

"Naam, bwana."

Nikasema, "Bwana, nataka kukuuliza swali."

Akasema, "Endelea moja kwa moja."

Nikasema, "Ulipo upanda ule mti pale, ulikuwa mkubwa kiasi gani?"

"Loo," akasema, "lilikuwa ni chipukizi tu, yapata urefu *huu*."

⁴⁵ "U-huh." Nami nikasema, "Nataka kukuuliza, sasa hivi ni juma la mwisho la Agosti, hata hatujawa na usiku baridi, lakini matofaa yote yameanguka kutoka kwenye mti huo, na umepukutisha majani yake, jani hilo limerudi chini mizizini."

"Hiyo ni kweli."

Nikasema, "Bwana, kwa nini hilo jani likaanguka? Lilinyauka?"

“La.” Akasema, “Vema, uhai uliliondokea.”

“Loo, kumbe. Halafu uhai ukautoka, ukarudi mzizini?”

“Naam.”

Nikasema, “Bwana, kama haukurudi mzizini, ingekuwa?”

⁴⁶ “Vema,” akasema, “huo mti. . . Hauna budi kurudi mzizini, huo mti usingeishi, ungekufa, baridi kali ingeuua.” Kasema, “Inafikia ishirini na thelathini chini ya sufuri huku chini wakati mwingine.”

⁴⁷ Nami nikasema, “Um-hum.” Nikasema, “Bwana, niambie ni Akili gani inayouambia huo utomvu uondoke kwenye huo mti, na uingie mizizini kwa ajili ya baridi kali. Sasa, hebu weka ndoo ya maji kwenye ile nguzo *pale* nje, uone kama katikati ya Agosti, maji yataanza kushuka chini ya hiyo nguzo.” Nikasema, “Mti hauna akili, haujui majira, hauna akili. Hata hivyo, kuna Akili fulani mahali fulani inayourudisha mti huo upate kuhifadhi uhai wake.”

Akasema, “Sikuwa nimewazia hilo namna hiyo.”

⁴⁸ Nikasema, “Basi unaliona papa hapa uani mwako. Kwa nini ungetaka kumwona mhubiri huyo basi, wakati unaliona papa hapa?” Nikasema, “Akili ile ile iliyoniambia ya kwamba dada ya mwanamke huyo alikuwa akifa kwa kansa, na katika ono nikamwona ameponywa, Akili iyo hiyo iko karibu sana nawe, mpaka inaudhibiti mti ulio uani mwako.”

⁴⁹ Akasimama na kunipa mkono, nikamwongoza kwa Kristo alasiri hiyo, akafa yapata mwaka mmoja baadaye. Nilikuwa huko chini mwaka huu nami nikakutana na mjane wake, nilipanda kwenda kumwomba nikawinde. Alikuwa akitaka kunifukua mahali hapo kwanza, niliporudi kule. Nikasema, “Ngoja kidogo tu.” Yeye hakuwako nilipokuja kule.

Akasema, “Bwana, kwani huwezi kusoma?”

Nikasema, “Naam, mama.” Nikajongea. Nikasema, “Hivi hunijui mimi?”

Akasema, “La, bwana, sikujui. Hizo leseni za Indiana kwenye gari hilo?”

Nami nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham. Mume wa- . . .”

⁵⁰ “Loo!” Akaanza tu kulia, na kuinua mikono yake juu, na kuanza kumsifu Mungu. Akasema, “Mwanangu, unaweza kuwinda popote utakapo, ukae kadiri utakavyo.”

⁵¹ Ilikuwa ni kitu gani? Kitendawili. Hakuna ajuaye, hakuna. Huwezi kupata Akili inayotawala Maumbile ya Ulimwengu, bali ni kitendawili, hatuwezi kulielezea.

⁵² Nilikuwa nikiwazia juu ya mauti, na kama tuko kwenye majani, jani huning’inia juu ya mti kutimiza kusudi fulani, nami na wewe tunaning’inia kwenye Mti wa Uzima baada ya kumkubali Kristo. Na baada ya kitambo kidogo, majira

yatakapobadilika, uhai huondoka kwenye jani hilo unaingia mzizini, unarudi tena mwaka ujao, ukileta jani jipya.

⁵³ Nasi Wakristo tunaomwamini Kristo tunao Uzima wa Milele, nasi tunaning'nia kwenye Mti wa Uzima, lakini siku moja jani hili la kale litaanguka, lirudi kwa Mungu aliyelitoa, ili tu kurudi katika msimu mwingine. Msimu huu tumegawanyika, sisi ni wanaume na wanawake, na yote hayo, ni msimu wa mbegu. Mti daima, mwaka baada ya mwaka, kutoa ushahidi na ushuhuda wa Mungu aliye hai . . .

⁵⁴ Jua huchomoza na kutua kuonyesha kuzaliwa, mauti, kufufuka, kuzaliwa, mauti, kufufuka, likigeuka kikamilifu. Majira ya kiangazi, baridi kali, kuchipua, kupukutika, yakionyesha tu kikamilifu mauti, kuzikwa, kufufuka, mauti, kuzikwa, kufufuka. Lakini tutakapojitokeza tena, itakuwa ni msimu mpya kabisa, itakuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu, hakutakuwako na mauti tena. Loo, tungeweza kukaa alasiri yote juu yake. Ni ajabu jinsi gani kuona vitendawili vya Mungu, kuona jinsi Yeye—Yeye anavyolifanya!

⁵⁵ Katika Waebrania, mlango wa 11 na kifungu cha 3, inasema mle ndani ya kwamba Mungu aliumba ulimwengu, aliuumba ulimwengu kwa vitu visivyoonekana. Dunia ii hii tunayokalia ni kitendawili. Ni kitu gani? Ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, wazia hilo. Kiti unachokalia, mahali unapoweka miguu yako ni Neno la Mungu lililonenwa. Yeye alikifanya bila kitu chochote cha kukitengenezea, Kitu pekee alichokuwa nacho kilikuwa ni Neno Lake, nalo Neno Lake Lenyewe ni Uumbaji. Mara linaponenwa, haliwezi kurudi tena mpaka litakapotimiza yale ambayo limekusudiwa. Haleluya!

⁵⁶ Daktari, ninaanza kujisikia kubarikiwa. Neno Lake haliwezi kurudi mpaka limetimiza yale yaliyonenewa. Mungu anawangojea alasiri ya leo watu ambao watalikamata Neno hilo na kulishikilia mpaka litakapotimiza yale lilivyokusudiwa. Naam, haliwezi kurudi, ni kitendawili, Neno lote la Mungu ni kitendawili, haliwezi kurudi, halina budi kutimiza yale yaliyonenewa.

⁵⁷ Sasa, kwenye somo letu, Yoshua. Unapoendelea kusoma mlango huo wote, utaona ya kwamba Biblia inasema ya kwamba hapajakuwapo na siku kama hiyo, hapo kabla au baadaye, ambapo Mungu alimsikiliza mwanadamu. Nina msichana tineja, Rebekah, yuko katika shule ya upili. Na hapa siku moja nilikuwa nikisoma hayo, naye akasema, “Baba, hapana shaka kuna kosa hapo mahali fulani.”

Nikasema, “Hakuna kosa. Hamna ninii . . . Hakuna makosa katika Neno la Mungu.”

Akasema, “Baba, ninii . . . Yoshua kamwe hakulisimamisha jua, Baba.” Nikasema . . . Akasema, “Aliisimamisha dunia.”

Nikasema, “Rebekah, alilisimamisha jua!”

Akasema, “Baba, asingeweza kufanya hivyo.”

“Vema,” nikasema, “unafikiri Neno la Mungu hukosea, Mpenzi?”

Kasema, “La, siamini hilo, Baba, bali ninaamini Yoshua kamwe hakuelewa.”

Nikasema, “Huku akimjua Mungu vizuri vya kutosha kufanya mwujiza kama *huo*, na hata hivyo ati hakuelewa? Alijua alichokuwa akizungumzia.”

Akasema, “Baba, jua tayari limesimama, halisogei, yeye aliisimamisha dunia.”

⁵⁸ Nikasema, “Hakuwa akizungumza kuhusu hilo kombora, alisema, ‘Simameni kimya juu ya Gibeoni; na katika bonde la Aiyaloni, tulieni,’ wala jua kamwe halikusogea kutoka Gibeoni, wala Aiyaloni kwa saa ishirini na nne. Hakuwa akizungumza juu ya lile kombora *huko* nje, alikuwa akizungumza juu ya jua kuivuka dunia. Hakuhusika na *hilo*, alihusika na mwangaza wa kutosha kumwangusha adui wa Israeli.” Jua ndilo alilokuwa akizungumzia, jua, uakisi wa jua, hilo ndilo jua alilokuwa akizungumzia.

⁵⁹ Neno la Mungu halikosei. Kile lisemacho, halihitaji yoyote, tafsiri ya mtu fulani kulipindua, kulifanya liseme jambo ambalo halisemi. Lichukue tu kama linavyosema, kwa sababu ni Neno la Mungu.

⁶⁰ Sasa, hata hivyo hilo likiwa pale, yule mwandishi aliyekandika Kitabu hiki na kusema hapajakuwapo na kitu kama hicho, Mungu yeye yule aliyelisimamisha jua alisema hivi katika Marko 11, 11:22 na 23, Yeye alisema, Yesu alisema, alipokuwa akinena juu ya ule mti, “Amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba hayo usemayo yatatimia, yatakuwa yako.”

⁶¹ Sasa, haikuwa tu kwa ajili ya Yoshua pekee, ilikuwa kwa ajili ya mwaminio yeyote anayeweza kuliadini Neno la Mungu. Kwanza, huna budi kuwa na nia sahihi na kusudi sahihi, sababu yake sahihi. Sasa, lakini ilikuwa ni kitendawili.

⁶² Tunajua, wengi wetu tunajua, nami nimeona, mimi mwenyewe, mambo kama hayo yakitukia, mambo ya uumbaji ambayo ninajua yametukia. Kule kutowezekana (Laiti ningalikuwa na muda mrefu wa kukaa juu yake, lakini sina.), kwa thibitisho la kisayansi la kutokuwezekana kwa uumbaji, ni Mungu Mwenyewe tu angeweza kufanya hivyo, maana Yeye ni Mungu. Mungu ambaye angeweza kufanya kitendawili pale, angali ni Mungu yeye yule leo hii ambaye angali anaweza kufanya kitendawili. Kweli.

⁶³ Wakati wa Nuhu, katika siku za Nuhu ilikuwa ni kitendawili. Mnakumbuka, hapakuwapo na mvua duniani

mpaka siku ya Nuhu, Mungu aliitia maji kwa chemchemi na kadhalika, lakini Nuhu akaanza kujenga safina. Alikuwa akifanya nini? Kabla hicho kitendawili hakijatukia, Nuhu alikifanyia maandalizi. Loo, hebu niseme alasiri ya leo, laiti sisi hapa leo tungalijiandaa tu kwa ajili ya kitendawili chetu! Yule anayeweza kuleta kitendawili yuko pamoja nasi. Mungu ambaye kazi Zake zote ni kitendawili, zimepita ufahamu, haziaminiki, bali ni za kweli, Yeye anaweza kuleta kitendawili.

⁶⁴ Nuhu alikifanyia maandalizi. Ningewazia kwamba katika wakati wake wa maandalizi kwamba watu walisema, “Sijui maskini mwendawazimu yule ana nini huko nje, huko juu akigongogonga ma—maskini merikebu ya mbao. Haijawahi kunyesha, ni . . . hakuna kitu kama hicho.”

⁶⁵ Ningewazia sayansi ingeweza kumjia Nuhu na kusema, “Angalia hapa, tuna vyombo ambavyo tunaweza kurusha kwenye nyota, wala hakuna mvua huko juu. Maneno yako yanawezaje kuwa kweli kamwe, ati itanyesha, huku hakuna maji huko juu?” Lakini mnaona, kama Mungu amesema itanyesha, Yeye anaweza kufanya mvua. Kwa hiyo akajitayarisha kwa ajili yake, akatayarisha kite- . . . kitendawili, ndipo ikanyesha.

⁶⁶ Ibrahimu, wakati alipokuwa juu ya mlima pamoja na mtoto wake wa pekee, mtoto Isaka, alikuwa amengoja miaka ishirini na mitano kumpata huyo mtoto, na halafu, wakati huyo mtoto alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na minne, Mungu alimwambia . . . Alikuwa akifanya hivi kwa sababu gani sasa? Kuthibitisha ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake, haidhuru linaonekana lisilo la busara jinsi gani, Yeye angali anaweza kutenda na kufanya kitendawili.

⁶⁷ Akasema, “Mchukue huyu mvulana wako mdogo, mwenye umri wa miaka kumi na minne, umpandishe mlimani, kisha umtoe dhabihu.” Naye akampandisha mlimani.

⁶⁸ Na sasa, kama huyo . . . yeye akiwa na umri wa kama miaka mia moja na kumi na mitano wakati huo, alimngojea mvulana huyo miaka ishirini na mitano, na hapa mvulana huyo . . . naye alikuwa anaenda kuharibu ushahidi pekee alio nao wa kuiona ahadi hii ya Mungu, kuwa baba wa mataifa, kuwahi kutimia, na ndipo anaombwa kuuangamiza huo. Hiyo ndiyo sababu alipaita mahali hapo, “Yehova-yire,” kwa maana alipokuwa karibu tu tayari kumtii Mungu kikamilifu, Roho Mtakatifu akaushika mkono wake, ndipo kondoo dume akalia nyuma yake, huku amenaswa pembe zake nyikani. Ilikuwa ni kitu gani? Kitendawili.

⁶⁹ Angalieni, alikuwa kwenye safari ya siku tatu kutoka nyumbani kwake, huko nyuma miongoni mwa wanyama mwitu, na isitoshe, juu ya mlima ambapo hakungeweza kuwa na kondoo, wala asingeweza kuwa huko juu ambako hakukuwako na maji. Huyo kondoo dume alitoka wapi? Haikuwa ni ono, alimwua huyo

kondoo dume, na damu ikamtoka. Ilikuwa ni Mungu, Muumba. Kwa sababu alidumu katika wajibu wake kwa Neno la Mungu, kukaja kitendawili, naye akamwua huyo kondoo dume, akafa mahali pa mwanawe, kitendawili.

⁷⁰ Hakika ilikuwa ni kitendawili huko Sodoma, kidogo kabla ya wakati huo, wakati Sara alipoicheka Sauti ya Mtu katika mwili wa kibinadamu huko nje, ambaye alikuwa ni Mungu, Naye alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, Malaika huyo alielekeza, Naye akanena na Ibrahimu, na kumwita jina lake, “Ibrahimu” akamwita Sara, “Sara,” wakati alipokuwa amepokea jina hilo siku chache hapo awali, na kusema, “Ibrahimu, kwa muhula wake nitakurudia,” ndipo Sara, hemani, akachekeka, naye Malaika huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, si—si mmoja wa hawa, kama tu Theofania, alikuwa ni Mwanadamu ameelekeza mgongo wake kwenye hema, kasema, “Kwa nini Sara akachekeka hemani, akisema, ‘Hili haliwezekani?’” Ilikuwa ni kitendawili.

⁷¹ Wakati mmoja wakati majeshi ya Israeli yalipokuwa yamesimama yameshindwa, na kulikuwako na askari wakuu pale, watu wenye nguvu, Yoabu, Sauli, tangu kichwa na mabega kwenda juu mrefu kuliko kila mtu aliyekuwa naye jeshini, wote wamevaa silaha kubwa na panga, watu waliofunzwa, tangu ujanani, kupigana, lakini kwa sababu waliona upinzani mkubwa sana, waliogopa kukabiliana na changamoto ya Goliathi wa Wafilisti mwenye majivuno, waliogopa kukabiliana naye.

⁷² Lakini akaja maskini jamaa aliyeinama mabega, aliyeonekana mwekundu. Mama yake alikuwa ameoka mikate ya zabibu kavu, naye akaileta huko kuwapa ndugu zake. Basi wakati alipokuwa akizunguka-zunguka, akiwatafuta ndugu zake kambini, Mfilisti huyu alijitokeza na kujigamba, kasema, “Jichagulieni mtu, kisha aje huku apigane nami. Kama . . . Hatutakuwa na umwagikaji wowote wa damu kati ya mataifa.” Bila shaka hivyo ndivyo adui anavyopenda kujigamba, wakati anapofikiri ana uwezo kukushinda. Kasema, “Mleteni hapa, kisha tutachagua, nasi tutapigana, na halafu, nikimwua mtatutumikia, akiniua tutawatumikia.”

⁷³ Nanyi mwajua nini? Alisema hayo wakati usiofaa. Kulikuwako na maskini mvulana mdogo mle ndani, aliyeinama, mwekundu, Biblia ilisema, ambaye alikuwa amejua kile Mungu alichomaanisha, alikuwa amemwona Mungu katika matendo. Alijua ya kwamba Mungu wa Israeli alikuwa ni Mungu wa Milele. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemkomboa kutoka katika makucha ya simba, kutoka katika makucha ya dubu, kwa kombeo.

⁷⁴ Basi akawaambia ndugu zake, “Mnataka kuniambia ya kwamba ninyi Waisraeli wa majeshi ya Mungu aliye hai mtasimama hapa, na kumwacha huyo Mfilisti anayejigamba

aseme siku za miujiza zimepita? Mnataka kuniambia ya kwamba mtamwacha apite na hilo, wakati ahadi ya Mungu iko nyuma yetu?” Haleluya! “Ahadi ya Mungu iko nyuma yetu. Mnataka kuniambia mtamwacha ajigambe, na kusema?”

⁷⁵ Daudi alikuwa ndiye mdogo kuliko wote wa jeshi lote, wala hata hakuwa jeshini. Hakuwa amejiunga nao bado, kwa hiyo yeye—yeye alikuwa kwa namna fulani *mtoto*, hafai kitu, wala hakuwa mtu aliyefunzwa, hakuwa ameingia kwenye seminari bado, wala hakuwa na jaketi za kikanisa ambazo hao wengine walikuwa nazo, lakini, na walipojaribu kumvika moja, haikumwenea.

⁷⁶ Nami nafikiri, ni karibu jambo lile lile siku hizi, tunapovaa jaketi ya Sauli ya kikanisa, na kutwambia, “Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu,” halimwenei mtu wa Mungu. Kweli. Watu wa Mungu wanaamini katika kitendawili, wanamwamini Mungu.

⁷⁷ Naye maskini jamaa huyu mdogo alisimama pale, mabega yameinama, amejizungushia kipande kidogo cha ngozi ya kondoo, hana silaha kubwa, na kadhalika, kwa hiyo akasema, “Mnataka kuniambia mtamwacha Mfilisti huyo asiyetahiriwa, asiyeamini huyo aseme hakuna kitu kama hicho, na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai?” Kasema, “Nitaenda kupigana naye.”

⁷⁸ Ilikuwa ni kitendawili wakati mvulana mdogo aliposhindana na jitu lenye vidole vya inchi kumi na nne. Mtu asiye na upanga, ama asiye na ngao, kama walivyoweza kuona, akampa changamoto mtu aliyekuwa na mkuki kama sindano ya mfumaji, yapata urefu wa futi thelathini, ilikuwa ni kitendawili.

⁷⁹ Alifanya nini? Alisema, “Unakutana nami kama Mfilisti katika jina la Mfilisti, unanikabili kwa silaha, na kwa mkuki, na katika chuo kilichofunzwa, bali ninakabiliwa nawe katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli.” Jambo ndilo hilo. Na maskini mtoto mwekundu, mvulana, labda umri wa miaka kumi na sita au kumi na minane, akiwa na kombeo, akalua jitu hilo kubwa lililojigamba, kitendawili, kwa sababu alimtumainia Mungu. Bila shaka.

⁸⁰ Musa, baada ya kuwa mtu aliyefunzwa vizuri, mwanajeshi, akijua alichokuwa akizungumzia, alijua jinsi ya kulishikilia jeshi, alijua jinsi ya kupigana na alikuwa amezijaribu silaha zake, lakini hazikufaulu. Basi ilikuwa ni kitendawili, baada ya kuzungumza na Mungu katika mfano wa moto kwenye kichaka, kwamba alichukua fimbo kavu kutoka jangwani akashuka na kuliteka jeshi, akaliteka taifa kwa fimbo kavu. Akaliteka jeshi, akaliteka taifa akiwa na umri wa miaka themanini, bila kitu ila fimbo mkononi mwake. Haleluya!

⁸¹ Ilikuwa ni kitu gani? Haikuwa ni Musa, wala ile fimbo, Ilikuwa ni Mungu wa uumbaji katika hiyo, ndiye aliyekuwa akifanya jambo hilo, Mungu, katika maskini fimbo hii kavu, “Chukua fimbo hii mkononi mwako ushuke uende kule,” kama nilivyosema hivi majuzi usiku, uvamizi wa mtu mmoja.

⁸² Sasa, ambapo Musa alipata shida katika mwili na kumwua mtu mmoja, daima lilimlelea, bali alishuka akaenda kule katika Roho, na kuliua taifa zima, ilikuwa ni utukufu. Hakika. Yeye alikuwa akifuata amri za Bwana, hilo ndilo linalolitekeleza.

⁸³ Mara nyingi nimewazia jinsi hilo lilivyoonekana la kipumbavu kwa nia ya kimwili, mzee, masharubu yakining’inia kifuani mwake, labda kichwa chake chenye upara kiking’aa kwa jua, nywele zimeinama chini, akimvuta maskini punda mmoja nyuma yake, mkewe ameketi pale na mtoto mchanga ameketi nyongani mwake, fimbo hii kuukuu, macho yake yakiangalia juu moja kwa moja kuelekea angani, akishuka kupitia pale, “Kwani unaenda wapi, Musa?”

“Nashuka kwenda Misri kuiteka.”

⁸⁴ Jambo ni kwamba, aliiteka, kwa sababu angeweza kwenda katika Jina la Bwana. Mungu anahitaji tu mtu mmoja mkononi Mwake, Yeye anaweza kufanya hayo mengine. Amejaribu kutafuta watu. Wakati mwingine Yeye anaweza kumshika mtu mkononi mwake. Ndipo akashuka na kuteka taifa zima akiwa na fimbo mkononi mwake.

⁸⁵ Sasa, hebu niambieni tu kama hilo ni la kawaida, utaratibu wa kawaida, kwa mtu kuchukua kijiti mkononi mwake na kuvuka, kuiteka Urusi. Kama Mungu alimtuma, ataiteka, maana Mungu aliyemtuma atakuwa pamoja naye. Yesu alisema, “Kama vile Baba alivyomituma Mimi, nami nawapeleka.” Na wakati Yeye... Baba aliyemtuma alikuwa ndani Yake, na Mungu anapomtuma mtu yeyote, Kristo anaingia ndani yake, hakika, “Kama Baba alivyomituma Mimi,” Baba aliyemtuma aliambatana Naye, naye Kristo anayemtuma mtu huenda pamoja na huyo mtu. Mnaona? Kuna vitendawili tu kila mahali.

⁸⁶ Sasa, kijiti kikavu, bali alishuka na kuiteka, ni dhahaka jinsi gani, linaonekana la kigeni.

⁸⁷ Ilionekana ni dhahaka wakati hapakuwapo na kisima mahali popote. Huko chini mabondeni, kote kando ya vilima hata wasingeweza kupata harufu ya maji. Na mahali pakavu sana palipokuwapo jangwani palikuwa ni Mwamba ule wa kale. Nendeni huku nje jangwani, mwangalie mwone. Inaonekana kama huko nyuma chini ya kichaka kizuri, ama mahali fulani, kungekuwako na chemchemi ndogo. Ukishuka bondeni ambako maji yote hutiririkia, kisha uchimbe chini kule utapata maji upesi sana. Lakini Mungu alimtuma juu ya kilima kwenye kitu kilicho kikavu kuliko vyote kule. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, Yeye anapenda kuchukua kitu ambacho ni duni na

kuonyesha ya kwamba Yeye ni kitu. Kama ambavyo nimesema mara kwa mara, “Mungu huwachukua watu duni kuwafanya *maarufu*. Lakini watu wanapofikiri wao ni *maarufu*, basi wanakuwa bure machoni pa Mungu.”

⁸⁸ Sasa, tunaona ya kwamba Musa alichukua fimbo hiyo kavu na kuupiga Mwamba, na alipoupiga, maji yakabubujika. Sasa, hebu okota fimbo uende jangwani leo hii uanze kupiga miamba. Ilikuwa ni kitendawili.

⁸⁹ Ilikuwa ni kitendawili wakati Mungu aliposhusha mana kutoka mbinguni. Naam. Ilikuwa ni kitendawili. Hapana shaka...Sijui kama hakuwa na matanuri makubwa kule kuiokea. Haikumbidi kuwa nayo, Yeye alikuwa ni Muumba, Naye aliumba mana iliyoanguka mpya kila usiku. Haikumbidi kuwa na meko, Yeye ni Muumba.

⁹⁰ Wakati mmoja wakati mwaminio alipoingia kwenye kundi baya, tuna hao wakati wote, mwaminio, jina lake Yehoshafati, aliingia katika kundi baya pamoja na Ahabu, anayejifanya mwaminio. Na wakati anayejifanya mwaminio na mwaminio wanapokusanyika pamoja, una shida. Sasa, unapomwona mwaminio katika seminari iliyo na kundi la wanaojifanya waaminio mle ndani, una shida tena.

⁹¹ Kwa hiyo Yehoshafati alitaka kisingizio, ama, Ahabu, hasa, aliagizia Yehoshafati ashuke aje. Alimwonyesha utukufu wote wa ufalme wake, naye Yehoshafati, kama mwaminio, wakati mwingine akiona jambo la kuisimua, jambo lisilo la kawaida, anashikwa na msimko juu yake, na hapo ndipo huyo mtu hana budi kuwa mwangalifu. Hapo ndipo ninyi wasichana inawabidi kuangalia, maskini jamaa fulani aliyechana nywele zake chini, na, iweni waangalifu. Baadhi yenu wavulana inawabidi kumwangalia ma—maskini Yezebeli huyo mdogo, mwajua, akiwaongoza kwenye njia mbaya. Iweni waangalifu, dumuni katika kundi linalofaa.

⁹² Angalia, kwa hiyo huyu hapa mwaminio katika kundi la wanaojifanya waaminio, kwa hiyo alikuwa na lengo la kibinafsi, bila shaka, naye akasema, “Sasa, hebu nikwambie tutakalofanya. Unajua sisi ni ndugu, sisi sote tuko sawa.” Lakini sisi si sawa. La, bwana, huchanganyi mafuta na maji. La, bwana. “Sisi sote ni sawa tu, kwa hiyo magari yenu ya farasi yawe yetu, na yetu yawe yenu, nasi tutakwea twende Gilgali, na tutapigana vita hivi, na kuwasukumia mbali, hawa adui.”

Vema, Yehoshafati alikuwa na adabu ya kutosha juu yake kusema, “Hivi hufikiri inatupasa kumtaka shauri Bwana kwanza?”

⁹³ Ninaweza kuwazia Rais mkuu Ahabu akisema, “Ahem! Mbona, bila shaka. Hakika, sisi ni—sisi ni taifa kuu hapa, linalomwamini Mungu. Kwa hiyo wajua nini? Nimepata jibu hivi punde.” Loo, naam. “Nina seminari hapa chini iliyojaa hao, nina

manabii mia nne waliofunzwa vizuri sana nchini, nina walio bora kuliko wote. Unapaswa kuwasikia wakisema, 'Ah-man.' Unapaswa kusikia yale maombi madogo, matamu wanayoweza kuomba. Waleteni, hebu tuwaone."

⁹⁴ Kwa hiyo wakajivika wapate kufanya kitu cha kupendeza, wakasimama nje malangoni, basi walipofanya hivyo, pale, wakawaleta manabii mia nne, na walipofanya hivyo, wote hao ni manabii, nao wakasema, "Kwea, na Bwana akubariki. Kwea. Sisi ni mia nne kamili, kwa nia moja. Kwea, 'Nitakubariki, nitakuwa pamoja nawe.'"

⁹⁵ Lakini hilo halikumgusa Yehoshafati. Unajua, wanaweza kukwambia mambo haya yote ni sawa, lakini moja kwa moja moyoni mwako unajua. Kama nilivyosema jana, "Hiyo Sauti ndogo tulivu hulizungusha gurudumu lote." Jambo fulani halikuonekana sawa, akasema, "Bwana, hivi huna mmoja zaidi?"

⁹⁶ "Ati mmoja zaidi, wakati seminari nzima iko hapa?" Hum? "Mbona, huyu *hapa* Askofu Mkuu *Nanii* na hao wengine wote. Tayari amejitengenezea pembe za chuma, na kusema, 'Kwa *hizi* utamsukuma adui atoke nchini.'"

⁹⁷ Nayo, ilionekana, ilikuwa ni kweli kabisa, kwa sababu, kwa kweli, nchi hiyo ilikuwa ni mali ya Israeli. Mnaona, inaweza kuonekana halisi sana na sahihi sana, bali kama unataka kitendawili, inakubidi usiondoe hata nukta moja kutoka kwenye Neno la Mungu, huna budi kudumu moja kwa moja na Neno. Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Lakini ni kwa masharti.

⁹⁸ Sasa, ilionekana kama: "Nchi hiyo ni yetu, kwa nini tusiende tukaichukue? Ni yetu, ni mali yetu." Nao watu hao hawakuwa makafiri tu, walikuwa ni manabii wa Kiyahudi, wakasema, "Kwea, Bwana yu pamoja nawe." Lakini jambo ni kwamba, walichanganyikana na ulimwenguni. Wakati wa utawala wa Ahabu na Yezebeli, huyo mke alikuwa amewaongoza kote na—na kuwachanganyisha wote ulimwenguni, na, kwa kweli, Roho wa Bwana hakuwa pamoja nao.

⁹⁹ Kwa hiyo basi, aliwaleta tu huko nje nao wakatabiri. Lakini hata hivyo, hilo kwa namna fulani halikumridhisha Yehoshafati, akasema, "Hivi huna mmoja zaidi unayeweza kumtaka shauri?"

¹⁰⁰ Akasema, "Naam, nina mwingine, bali yeye ni mtakatifu anayejibingirisha. Kamwe si—simpendi, sikuzote ananikatakata." Mungu asifiwe! "Daima ananikemea. Anaamini nina mke mbaya kuliko wote ulimwenguni. Yeye—yeye—yeye—yeye ni mbaya sana. Kamwe hatuwezi kuwa naye hapa."

"Loo," akasema, "mfalme asiseme hivyo. Ningependa kumsikia."

¹⁰¹ Kasema, “Yeye ni Mikaya, mwana wa Imla. Lakini si—si—simplendi kabisa, daima anasema jambo baya kunihusu mimi, nimemfunga gerezani mara dazani moja. Lakini yeye ni mmoja wa hao watakatifu wanaojibingirisha. Lakini hatumtaki hapa juu.”

“Loo, mfalme asiseme hivyo. Agizia akaitwe.”

¹⁰² Kwa hiyo walikuwa na mtangulizi, wakati mwingine kama mnavyofanya mnapoenda kwenye uamsho. “Ah! Shh, lakini usiseme lolote kuhusu *hili*. Usihubiri dhidi ya jambo *hili*. Loo, ninii, hawaamini jambo *hilo*. Sasa, achana na *hili*. Sasa, usiseme lolote kuhusu *ahemu!*” Vema, mnajua ninachotaka kusema, siyo? “Usiseme lolote kuhusu *hilo* kwa sababu utaudhi, utaudhi hisia zao. Sasa, wana wachungaji kule, nao—nao wanawaambia *hili, lile*. Usininii . . . Wewe sema jambo lile lile.”

¹⁰³ Mikaya, mtu aliyetiwa mafuta, akasema, “Nitasema tu yale Mungu atakayoweka kinywani mwangu kusema.” Amina. Mungu, tupe Mikaya wengine zaidi. “Lakini mimi husema tu yale Mungu anayoweka kinywani mwangu.”

¹⁰⁴ Hebu tuone kama ono lake lilikuwa pamoja na Neno, hivyo ndivyo ilivyo . . . amueni, yaliyo kweli, angalieni ni lipi linalolingana na Neno. Mikaya akashuka akaja. Akasema, “Ninakuapisha mara ngapi?”

¹⁰⁵ Mikaya akasema, “Kwea. Kwanza nipeni usiku huu, hebu nione kile Bwana atakachosema, ndipo nitawaambia kilicho BWANA ASEMA HIVI.” Hiyo ni kweli. Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu. Hebu tuone kilicho sahihi.

¹⁰⁶ Kwa hiyo usiku huo Mikaya akaona ono naye akamwona Bwana. Naye akachunguza ono hilo kwa Neno, nalo lilikuwa sawa na Neno. Ono lolote, ndoto, ama chochote ambacho ni kinyume cha Neno, si sahihi.

¹⁰⁷ Hebu nisimame kwa dakika moja tu. Mtu fulani alinjia si muda mrefu uliopita, alitoka ng’ambo. Mtu huyo alikuwa amekosea, alikuwa na watoto watatu ama wanne, na mke, naye alikuwa akitembea na mwanamke fulani hapa, sisemi jambo lolote la utovu wa uadilifu, lakini kamwe halikuonekana sawa. Mnaona, inawabidi kuangalia mnalofanya mbele ya macho ya umma, ninyi ni nyaraka zilizoandikwa.

¹⁰⁸ Naye akasema . . . Kwa namna fulani nilimwuliza juu yake, nikasema, “Bwana, natumaini hufikiri mimi ni fidhuli, bali ningetaka tu kusema jambo fulani kama mhudumu. Hivi huwazii ya kwamba watu hapa watafikiri . . . ?”

“Loo,” kasema, “La, la, hilo ni sawa nchini mwangu.”

Nikasema, “Lakini huko nchini mwako,” unaona, “uko *humu*. Na kama . . . Watu watawazia jambo fulani kuhusu hilo.” Akasema . . .

Nikasema, “Je, unamfahamu huyo mwanamke?”

“Naam.”

Nikasema, “Je, unajua asili yake?” Niliijua.

109 Akasema. “Naam.” Kasema, “Ndugu Branham, najua anaishi sasa hivi pamoja na mume wake wa nne.” Kasema, “Na, Ndugu Branham, unajua nini? Yeye ni mwanamke mzuri sana.” Kasema, “Nilimwendea Bwana, nami nikasema, ‘Bwana, niambie mwanamke huyu ana shida gani.’ Kasema, ‘Kwa nini umbariki na Roho Mtakatifu, na kila kitu, huku anaishi katika uzinzi?’”

110 Akasema, “Vema,” kasema, “unajua, Bwana alinipa ndoto.” Kisha kasema, “Nilimwona mke wangu akiishi kizinifu na mwanamume mwingine.” Nami nikasema... Kisha kasema, “Ndipo akanijia, akaanguka chini, kasema, ‘Utanisamehe?’ Nami nikasema, ‘Hakika.’ Kisha kasema, “Ndipo Bwana akasema, ‘Namsamehe.’ Kasema, ‘Unaona, haijalishi kama amefanya jinsi anavyofanya, namsamehe.’”

111 Nikasema, “Bwana, ono lako, ama, ndoto yako ilikuwa tamu, bali haiambatani na Neno la Mungu.” Kweli! Mungu hawezi kusema Jambo moja, na kulighairi *hapa*. Hana budi kusema Jambo moja, na kudumu Nalo mpaka litakapotimiza yale liliyokusudiwa. Ndipo unaona kitendawili.

112 Kwa hiyo tunaona, na, Mikaya akasema, “Kwea, ukitaka, lakini niliwaona Israeli kama kondoo wametawanyika, bila mchungaji.”

113 Ndipo Zedekia akaja, ambaye ni nanii mkuu... kundi la walio wakubwa sana, mmoja wa manabii, ama aliyefaa sana, kiongozi wao, akaja na kusema, akampiga kofi kinywani, na kusema, “Roho wa Mungu alipitia njia gani kutoka... wakati alipotoka kwangu?” Hakuwa na Roho wa Mungu.

Akasema, “Niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo kilimani.”

114 Na kwa hiyo akasema, “Mchukueni mtu huyu,” mfalme alisema, “mkamtie gerezani, na kumlisha chakula na maji ya huzuni hata nitakaporudi kwa amani, kama vile wachungaji wangu wote hapa wasemavyo ya kwamba nitarudi, ‘Nawe utarudi kwa amani.’”

115 Sasa, kama Ahabu angaliketi chini na kusikiliza... Kumbukeni, tunajua ya kwamba Eliya alikuwa ni nabii aliyethibitishwa. Nabii haibuki tu usiku mmoja, manabii wanazaliwa manabii, hakika, naye alikuwa nabii tangu utotoni mwake. Naye, kila Neno alilosema, Fundisho lake lote lilikuwa ni la Mungu, kwa sababu Mungu alimthibitisha, kama alikuwa ni nabii, Yeye alimthibitisha.

116 Kwa hiyo basi wakati alipofanya hivyo, alijua basi, Mikaya aliona lile ono, nalo hilo ono lilikuwa linalingana na—na ono la nabii. Manabii wawili walikutana pamoja. Naye Eliya alikuwa

amemwambia Ahabu yale yatakayotukia, kwamba mbwa watairamba damu yake. Basi Mikaya angeweza kubariki kile Mungu alichokuwa amelaani?

117 Sasa, hebu nisimame kwa dakika moja. Mungu anaweza siku hizi kubariki kile alicholaani? Hawezi kufanya hivyo. Kusema uongo, kuiba, kudanganya, mambo haya yote ni makosa, na mambo mengine mengi ningeweza kusema. Kama ni makosa, ni makosa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

118 Nini kilitukia? Tunaona ya kwamba hicho kilikuwa ni kitendawili, kwamba mtu mmoja, maskini mtakatifu mmoja anayejibingirisha aliyevaa ovyoovyo, alisimama hapa mbele ya seminari nzima ya manabii, na Mungu akathibitisha Neno lake kwa sababu alikuwa pamoja na Neno. Hiyo ni kweli. Ni... ilikuwa ni kitendawili.

119 Wakati Mungu alipomchukua Yohana Mbatizaji na kumfanya mtangulizi wa Kristo, badala ya kumchukua mmoja wa makuhani tajiri, wa kifalme, ilikuwa ni kitendawili. Mungu angeweza kumchukua mtu ambaye hakuwa na elimu hata kidogo? Alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa wakati amewapoteza wazazi wake, akakaa huko nje nyikani, akatoka, alionekana kama mdudu aliyejaa manyoya, hizo ndevu usoni mwake, naye amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, na kusimama kwenye matope kule juu, na kuita ku—kusanyiko alilokuwa akihubiria kizazi cha nyoka nyanini. Ungeweza kuwazia Mungu akimchukua mtu ambaye angelisema hivyo kwa kusanyiko la Wayahudi wastaarabu, waliodhaniwa ni waaminio?

120 Akasema, “Enyi uzao wa nyoka!” Sio, “Halo, Askofu *Nanii*, nina furaha sana kukuona.” Loo, ewe dondoadume...! “Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo? Msiwazie, ‘Sisi ni wa *hili* ama *lile*,’ Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Wakati Mungu alipolithibitisha, ilisababisha kitendawili. Alimwona Roho Mtakatifu akishuka kama hua juu ya Mwana wa Adamu, ilikuwa ni kitendawili.

121 Ni kitu gani kilichokuwa kitendawili zaidi ya kuzaliwa na bikira? Sasa, ninajua mimi si...sitaki...Sasa, tuna kusanyiko lililochanganyika. Sasa, ninawatakeni mnielewe, kwa kuwa ninatarajia jambo fulani, na kutarajia jambo fulani, huna budi kudumu na Neno. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo.” Hayo ndiyo masharti. Sio, leo, na kesho kitu kingine, na kupindua kwa sababu ya *hili*, na kupindua kwa sababu ya *lile*, bali dumu moja kwa moja na Neno na Kalvari, kisha uombe utakalo.

122 Sasa, tunaona ya kwamba katika huku kuzaliwa na bikira, wengi wa watu, ninyi Wakatoliki wa thamani, asili yangu ni

Katoliki pia, mwajua, kwa hiyo tunaona ya kwamba siku hizi mnamchukua Mariamu na kumfanya mungu mke, mwombezi.

¹²³ Ndugu Valderna, hapa mahali fulani jukwaani, ninaamini, alikuwa huko chini Meksiko, Jemadari, [Ndugu mmoja anasema, “Medina.”—Mh.] Medina, Medina. Alikuwa hapa hivi majuzi usiku, akanikumbatia kwa mikono yake, na kuzungumza kupitia mkalimani wake, akasema, “Ndugu Branham, ninavutiwa na ujasiri wako wa kusimama kwenye imani yako.” Kasema, “Kaa nayo, mwanangu.” Yeye ni mtu, mwanajeshi, anayejua maana ya kutoa amri, alisimama huko nje kwenye mstari wa mbele, “Wewe kaa kwenye kituo chako!” Hivyo ndivyo Mungu anavyowataka askari Wake wafanye, wasimame kwenye wajibu wao bila kujali kijacho wala kiendacho, wakae hapo, wakae papo hapo. Kwa hiyo akasema. . .

¹²⁴ Kuzaliwa huku na bikira. . . Nilikuwa huko chini Meksiko kule, na kulikuwako tu na watakatifu wa kila namna. Huko ndiko maskini mtoto huyo mchanga alipofufuliwa kutoka kwa wafu, mliliona katika Wafanyabiashara Wakristo. Ninataka kuwashukuru kwa ajili ya pongezi hizo, Mungu awabariki. Wakati huyo mtoto mchanga, tusingeliacha liende namna hiyo tu, mpaka daktari aliposema ya kwamba mtoto huyo alikufa asubuhi hiyo saa tatu, na hii ilikuwa yapata saa nne ama tano usiku huo. Naye maskini huyo dada amesimama huko nje, maskini msichana Mkatoliki aliyekuwa na mtoto mchanga mkononi mwake, wala mabawabu mia tatu wasingeweza kumzuia asiende jukwaani.

¹²⁵ Billy alinjia, kasema, “Baba, huna budi kufanya jambo fulani kuhusu hilo,” kasema, “ha—hakuna lingine.” Kasema, “Hana kadi ya maombi,” kasema, “kwa sababu nimeangalia.” Kasema, “Huyo ndugu, sijui. . .”

¹²⁶ Samahani, enyi Wameksiko, bali nilimwita *Mañana*, ambalo linamaanisha “kesho,” Mnaona? Alipaswa kuja kunichukua saa moja naye akaja saa tatu, sikuzote, hucheleva kwa yapata saa mbili ama tatu, yeye ni mbaya kama nilivyo mimi. Halafu basi, huyu hapa, alikuwa akisambaza kadi za maombi, naye angetembea pamoja na hizo zote, mwajua, huku Billy akimwangualia, kuhakikisha ya kwamba hakuza moja, kwa hiyo, akimwangualia, huku akitembea. . . Iweni waangalifu, nilimtuma huko chini kufanya hivyo. Kwa hiyo aliheshimu hilo.

¹²⁷ Kwa hiyo ningeingia jukwaani. Usiku uliotangulia, huko, maskini ndugu mmoja Mmeksiko alikuwa amekuja. Na kitita kizima, lundo, lililojaa nguo kuukuu usiku huo. Maskini, mzee Mmeksiko, na maskini miguu michafu, yapata umri wa miaka themanini, kipofu kabisa, kofia kuukuu mikononi mwake iliyoshonwa kwa kamba ya kitani, imejaa mavumbi, naye alikuwa akienda pale akisema jambo fulani katika Kihispaniola, nami nisingeweza kumweleva. Na kwa hiyo, alikuwa akijaribu

kunifikia wakati alipogundua...Akaingiza mkono mfukoni mwake, akatoa rozari na kuanza, haina haja. Alikuwa kipofu, nami nikamvuta huyo mzee karibu nami.

¹²⁸ Nilifikiri...Mwajua, huna budi kuhisi hali ya huyo mtu, la sivyo kamwe hutamsaidia. Huna budi kuingia katika mateso yao, usipoingia, kwa moyo baridi tu, kamwe haitafanikiwa. Inakubidi kujiweka mwenyewe...Nikaangalia, yeye... Nikawazia, “Maskini jamaa mzee, labda yuna genge kubwa la watoto wadogo hapa nje mahali fulani.”

¹²⁹ Na uchumi wao ni duni sana, na hiyo ni kweli. Labda Pancho anapata peso thelathini kwa juma, naye ni mwashi, na huyo mwingine anapata peso kumi na tano, Pedro, na—naye ni mtu wa mikono, na—na ana kundi la watoto wa kuwalisha. Halafu basi, wanakula tortila ya mafuta mahali fulani iliyoookwa kwa saladi ya ameba, na vitu walivyotupa, bali hana budi kuweka akiba kiasi *fulani* kununua taa ya grisi aende kwenye madhabahu ya dola milioni moja kwa ajili ya dhambi yake. Upuuzi! Kristo ndiye Dhabihu yetu, Kristo Ndiye. Hatuhitaji madhabahu ya dola milioni moja, tunahitaji moyo ulio wazi.

¹³⁰ Kwa hiyo maskini mwanamke huyo kule chini, Billy akasema...Na, kwanza kuhusu mzee huyu, niliina mguu wangu kuona kama viatu vyangu...mimi huyo nimesimama pale nimevaa jozi ya viatu, labda kamwe hajapata kuwa jozi moja, nikawaza, “Endapo viatu vyangu vingemwenea, nitampa.” Nikaweka mabega yangu karibu na yake, alikuwa mkubwa zaidi, kwa hiyo nisingeweza kumpa nguo zangu.

¹³¹ Nikamkumbatia, nikawaza, “Kama baba yangu angaliishi, angekuwa na umri kama huo.” Nami nikasema, “Ee Bwana Mungu,” yeye, Ndugu Espinoza, labda yuko hapa mahali fulani, kamwe hafasiri maombi, nami nikaomba, “Bwana Mungu,” ndipo nikamsikia akisema kwa sauti kuu, “Gloria a Dios!” Naye akaangalia kote, angeweza kuona vizuri kuliko mimi. Alikuwa...angeweza kuona, naye huyo akaenda akipiga mayowe.

¹³² Kesho yake usiku, shali kuukuu na makoti yalilundikana namna *hiyo* kote jukwaani. Ndipo Billy akaniambia, akasema, “Baba, huwezi kumzuia mwanamke huyo kule,” akasema, “ana mtoto aliyekufa.” Mvua ikinyesha, nao walikuwa wamesimama pale, hakuna mahali pa kuketi, mahali hapo pakubwa, hakuna mahali pa kuketi chini, wakiegemeana tu tangu saa tatu asubuhi hiyo, na hii ilikuwa yapata saa nne na nusu usiku huo, wakisimama kwenye jua hilo na mvua. Loo, Marekani, Marekani, jinsi siku moja mtafika nchani mwa pembe isipokuwa mtubu. Hiyo ni kweli. Mungu mwenye upendo! Usiku huo niliona yapata watu elfu ishirini na tano wakimjia Kristo wakati mmoja, huko kwenye Jiji la Meksiko.

133 Ndipo mimi, nikamwona maskini mwanamke huyu, kule chini akipiga mayowe, mabawabu wangejaribu kumzuia, angempachika mtoto huyo chini ya mkono wake na kukimbia moja kwa moja katikati ya miguu yao. Wangejaribu kumshika, angeruka juu yao, apande juu yao, akiwakwaruza, akijipigania, kila kitu apate kupanda kule juu. Nao wakasema, “Huwezi kupanda juu,” wakamrudisha nyuma.

134 Kwa hiyo nikamwambia Ndugu Jack Moore, sijui kama alikuwa humu mkutanoni, nikasema, “Ndugu Jack, nenda kule ukamwombe. Yeye hanijui, kwa hiyo mwombe mtoto huyo mchanga, na hilo litamkomesha.” Nami nikageuka nyuma, nilikuwa namna *hii*, nikageuka kuangalia, nami nikaona katika ono, papa hapa mbele yangu, maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko, mwenye ngozi nyeusi, asiye na meno, akitabasamu. Nikangoja kidogo, nikarudi nyuma, nikaangalia tena, nikasema, “Ngoja kidogo,” kitendawili, “mleteni hapa.” Mabawabu wakafungua mstari.

Akaja pale, akaanguka chini, akaanza kupiga makelele, “Padre!”

135 Nikasema, “Hebu kidogo. Amka.” Nikasema, “Baba wa Mbinguni, sijui hilo lilimaanisha nini, lakini chini ya blanketi hili,” nalo limelowa maji, “kuna mtoto mchanga, aliyekufa. Walisema alikufa asubuhi ya leo saa tatu. Na maskini moyo wa mwanamke huyu una shauku, huyo ni mtoto wake mchanga. Ninamwekea mikono yangu kwa kutii ono hilo.” Yapata wakati huo huyo mtoto akafanya “Ng’wee,” naye akapiga mayowe, ana kuanza kupiga makelele, akafufuka, ilikuwa ni kitendawili.

136 Nikasema, “Ndugu Espinoza, usiandike hilo. Nenda kwa daktari upate taarifa iliyotiwa sahihi, ‘Mtoto huyo alikufa.’” Naye akafanya hivyo. Mnaona? Kitendawili. Nimeona hilo likitukia mara tano sasa, mara tano, kitendawili.

137 Kuzaliwa na bikira kulikuwa ni kitendawili. Siamini ya kwamba Yesu alikuwa sehemu yoyote ya Mariamu, huyo hakuwa mama Yake, ilikuwa ni mwanamke ambaye Mungu alimtumia kwa kusudi hilo, kama, kiangulio, kumzaa Mtoto Wake. Kama Mariamu . . . Kama uzao wa mwanamke . . . Ambapo, yeye ni yai na mwanamume ana himoglobini, kama hiyo ni kweli, Daktari, unaona, da—damu. Uhai uko kwenye seli ya damu.

138 Naye kuku anaweza kutaga yai, bali kama hajawa pamoja na ndege wa kiume, kamwe halitaanguliwa. Sasa, mara nyingi nimesema jambo hili, ninalisema tena: Majira ya kuchipua yanakuja, ndege wote watakuwa wakijenga viota vyao. Maskini mama ndege anaweza kuingia kwenye kiota chake na kuyalalia hayo mayai, na kukaa humo mwaminifu sana mpaka nusura afe kwa njaa, anakuwa myonge sana hawezi kuruka kutoka kwenye hicho kiota, hayo mayai kamwe hayataanguliwa, iwapo hajawa pamoja na mwenziwe.

¹³⁹ Sasa, ndugu, hakuna kitu kibaya na Waepiskopalia, Wamethodisti, ama Wabaptisti, lakini tuna nini? Maadamu ni dhehebu (Acha liwe ni la Kipentekoste.), kama hao watu hawajakutana na yule Mwenzi, Yesu Kristo, huna kitu ila kiota kilichojaa mayai yaliyooza yatakyokaa papo hapo na kuoza. Sijali ni Ph.D. ngapi, LL.D, L. maradufu D, ama chochote kile unachowabandika katika seminari, hivyo ni vya ulimwengu tu. Hatuna budi kupata Seli Zazi ya Uzima, Uzima wa Milele wa Mungu ulionenwa, “Mtu asipozaliwa mara ya pili . . .”

¹⁴⁰ Mna nini? Mnawafanya mashemasi, maaskofu, na kila kitu kingine, hamna chochote ila lundo la mayai yaliyooza, jambo pekee la kufanya ni kusafisha hicho kiota na kuanza upya tena. Sawa. Kamwe halitaweza kufanya hivyo mpaka tutakapoanza. Mnataka kitendawili? Mnataka Uzima? Hamna budi kuleta Uzima ndani yake. Hiyo ni kweli.

¹⁴¹ Mariamu, kama mwili wa Mtoto huyo, ambapo mwili unatokana na yai, na kama mwili wa Mtoto huyo ulikuwa ni wa Mariamu, basi nini? Basi ilimbidi Mariamu ashikwe na namna fulani ya mhemuko. Mnaona mahali mnapomweka Mungu akifanya? Mungu aliumba hilo yai na Seli hiyo ya Damu pia. Na Yeye hakuwa Myahudi, wala hakuwa Mmataifa, alikuwa Mungu, Mungu katika umbo la mwili wenye dhambi. Hiyo ndiyo sababu, “Sitaona . . . sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala kuiacha Nafsi Yake katika kuzimu.” Yeye alikuwa ndiye dhihirisho, Mungu, kuingia katika maskani aliyoiumba Mwenyewe. Yesu kamwe, katika Maandiko yote, hakumwita, *mama*, Yeye alimwita, *mwanamke*, si, *mama*, *mwanamke*.

Kasema, “Mama Yako yuko nje akikutafuta.”

¹⁴² Akasema, “Mama Yangu ni nani?” Akawaangalia wanafunzi Wake, kasema, “Yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu ndiye mama Yangu.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo mnaona, ilikuwa ni kuzaliwa na bikira kabisa, pande zote mbili, kuzaliwa na bikira. Kitendawili hakiwezi kuelezewa, hakuna kitu kinachoweza kukielezea.

¹⁴³ Hapa siku moja nilikuwa milimani nikiwinda, kulikuwa na maskini jamaa mkubwa, mrefu jina lake Jeverez, G-e-v-r-e-z, Mfaransa, tulikuwa tukirudi, nami nilikuwa tu nimekutana naye, ndipo akasema, “U nini wewe?”

Nikasema, “Mimi ni mhubiri.”

Akasema, “Unaonekana kuwa na akili kupita hiyo.”

Nami ni—nikasema, “Vema, mimi . . . Hayo ni maoni tu.”

Naye akasema, “Nadhani unaamini ya kwamba Mtoto huyo ali—alizaliwa na bikira.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Bwana, hilo ni kinyume na kanuni zote za kisayansi.”

144 Nikasema, “Huwezi kumthibitisha Mungu kwa sayansi, inakubidi kumwamini.” Humthibitishi Mungu, unamkubali, unamwamini. Kama unaweza kulithibitisha, si imani tena, basi ni jambo ambalo unaweza kulielezea, Mungu hawezi kuelezewa.

145 Kisha akaendesha mbele kidogo, akasema, “Siamini hilo, hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kunifanya niamini.” Kasema, “Yusufu alikuwa ndiye baba ya Mtoto huyo mchanga.”

Nikasema, “Mungu alikuwa ndiye Baba ya Mtoto huyo mchanga.”

Kasema, “Hakuna Kitu kama hicho.”

Nami nikasema, “Loo, upuuzi.”

146 Akasema, “Angalia, Bw. Branham.” Akasema, “Kabla hujalima mahindi, kabla hujakuza mti, ama chochote kile, hapana budi pawe na mgusano halisi wa wa kiume na wa kike kabla halijawezekana.” Kasema, “Huwezi kufanya hivyo, haiwezi kuzaa bila mgusano halisi.”

147 Nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani basi. Uliniambia ya kwamba mtu huyo alitoka kwenye,” akifundisha maadili ya Darwin, “mtu huyo alitoka kwenye seli moja ambayo ilikuwa ni kiwavi mdogo ama kitu fulani kilichogeuka kuwa sifongo, halafu kiwavi, na kisha kikakua, kisha ikaotesha dutu kidogo, ndipo mkono ukatokea, na kadhalika, yote namna hiyo.” Nikasema, “Basi mnadai ati huyo alikuwa ndiye mtu wa kwanza?”

Akasema, “Ninaamini hilo.”

148 Nikasema, “Imani yangu haina nguvu hivyo, bwana.” Nikasema, “Nisingeweza kuamini hilo, Ninaamini tu yale Mungu aliyosema juu yake, mnaona, ya kwamba Yeye alimwamba mtu kwa mfano Wake Mwenyewe.” Nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani basi. Kama... Utakubali ya kwamba—ya kwamba mwanamke huyu angeweza kumpata huyo Mtoto, bali ilimlazimu kuwa na mgusano halisi na mwanamume?”

Kasema, “Naam, bwana, ni kinyume na kanuni zote za kisayansi.”

149 Nikasema, “Basi ninataka kukuuliza jambo fulani.” Mnajua, Mama sikuzote aliniambia, “Mpe ng’ombe kamba ya kutosha, atajinyonga.” Basi nikasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani basi, mtu wa kwanza alitoka wapi ambaye hakuwa na baba wala mama? Huyo alitoka wapi?” Hajanijibu bado. Halina jibu. Mungu alimwamba mtu wa kwanza. Mungu ni Mwumba. Ni kitendawili.

¹⁵⁰ Sina budi kuharakisha, enyi marafiki, kuharakisha sana. Loo, jamani! Inakuwaje hayo...? Kwani wakati wote huenda wapi? Ninataka kukutana nanyi kote huko Ng'ambo ambako ninaweza tu kukaa kwa miaka milioni moja na kila mmoja wenu, tutazungumzia mambo haya.

¹⁵¹ Angalieni, wakati mmoja kulikuwako na m—mtu, Oral Roberts alizungumza juu yake hivi majuzi usiku, Samsoni, mtu wa kawaida tu. Nitakuwa mwenye dhahaka kuliko yeye, yeye hakuwa, ninii tu, mtu wa kawaida, alikuwa tu ni maskini mduvi mdogo, maskini jamaa mdogo. Kama mtu alikuwa na mabega kama mlango wa ghala, isingekuwa kitu kumwona akimwua simba.

¹⁵² Lakini maskini mduvi huyu, mwenye nywele za kipilipili, vishungi saba vidogo vikining'inia kichwani mwake, naye alikuwa akitembea huko nje, maskini mvulana wa mama, naye huyu hapa akitembea huku na huku kama maskini dondoadume, na muda si muda mwajua, Wafilisti elfu moja wakamshambulia.

¹⁵³ Sasa, kama umewahi kuona vazi la Wafilisti, laiti ningalikuwa na wakati wa kulielezea, lakini chapeo hiyo ina unene wa kama inchi moja na nusu ya shaba tupu juu ya kichwa chake. Sasa, kumbukeni, wangeweza kuitia shaba matiko siku hizo, ambalo hatuwezi siku hizi, maana Sulemani alikuwa na wembe, ulikuwa wa shaba. Sasa, angalieni, ile chapeo ya shaba, na mwilini mwake mwote kulikuwa na shaba nene aliyozungushiwa, ili aweze kutembea amevaa silaha zake.

¹⁵⁴ Eflu moja ya hao waliofundishwa, na hapa wakakutana na mtumishi wa Bwana huko nje, maskini mduvi mwenye nywele za kipilipili, labda amevaa jaketi ndogo, lakini Roho wa Bwana akamjia, naye akaokota mfupa wa taya la nyumbu, na kuwapiga Wafilisti elfu moja. Naam.

¹⁵⁵ Mbona, ndugu, maskini mfupa huo uliooza, wa taya la nyumbu huyo, ungepiga moja ya hizo chapeo kubwa za shaba nao, mbona, ungalipasuka vipande elfu moja. Hakika, lakini ilikuwa ni kitendawili, Mungu alikuwa kwenye maskini mfupa huo wa taya. Kama anaweza kuingia kwenye uliokufa, hakika anaweza kuingia kwa yetu iliyo hai. Angalieni, kitendawili, hakika ilikuwa. Naye akachukua mfupa huo wa taya na kupondaponda hizo chapeo moja kwa moja namna *hiyo*, mpaka akawapondaponda Wafilisti elfu moja, kitendawili.

¹⁵⁶ Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, alitembea juu ya maji, nielezeeni hilo. Niambie kisayansi jinsi mtu anavyoweza kutembea juu ya maji, kitendawili. Siku moja alichukua biskuti tano na samaki wawili na kuwalisha elfu tano. Yeye aliachilia atomi ya namna gani? Sasa, hao hata hawakuwa samaki hai. Wakati alipoumega mkate huo, akauvunja kutoka kwenye kipande cha biskuti, wakati alipozisambaza, kufikia wakati alipourudisha mkono Wake tena, kulikuwa na biskuti nyingine

pale, tayari imetokeza, ile ngano shambani, tayari imepikwa, grisi yote ndani yake, imekolea. Hiki *hapa* kipande cha samaki, Yeye akakivunja, na kipande kingine cha samaki *aliyepikwa*. Amina. Haleluya!

¹⁵⁷ Elementi hiyo tumepewa sisi, iwapo tu tutadumu katika Neno. Kaeni humo, naamini tuko ukingoni mwa kuliona likitukia. Ishi tu mwaminifu kwa Neno. Haya basi. Alikuwa na samaki waliopikwa, hicho kilikuwa ni kitendawili.

¹⁵⁸ Ilikuwa ni kitendawili wakati alipoenda kulichagua Kanisa Lake, kwamba aliwachagua wavuvi badala ya makuhani. Hiyo ni kinyume na maumbile. Inaonekana kana kwamba angekuwa na kanisa kubwa mno, pamoja na kundi lote la wahudumu waliopambwa na kustaarabika, na wanaojua theolojia yao, nao wana Ph.D. zao zote, na kila kitu. Hapo ndipo Yeye alipofikia. Lakini Yeye alipita tu kundi hilo lote, mnaona, akashuka na kuwachukua wavuvi ambao hata wasingeweza kuandika jina lao wenyewe. Biblia ilisema ya kwamba Petro na Yohana walikuwa wasio na elimu wala maarifa, hao ndio aliowachukua kwa ajili ya Kanisa Lake, hicho ni kitendawili. Bila shaka. Naam, bwana. Aliwachagua wavuvi, badala ya watu. . . badala ya makuhani.

¹⁵⁹ Sasa, tunaona ya kwamba kwenye Siku ya Pentekoste, ni ajabu kwamba alichagua kundi la watu wasio na elimu, na kuwatuma huko juu pamoja na agizo huko Pentekoste, si kwenda kwenye seminari fulani, bali wangoje hata watakapovikwa Uwezo utokao Juu. Kama mtu huyo, Petro, na Yohana na hao wengine, walitaka kuhubiri nao walikuwa wasio na elimu wala maarifa, inaonekana kama angeninii, angesema, “Enyi vijana, kuna shule nzuri papa *hapa*, nendeni mpaka mtakapojifunza ABC zenu, ndipo baada ya kufanya hivyo, mtaingia shule yenu ya sekondari, mpate yote, hayo yote, ndipo mtachukua miaka minne ya shule ya upili, kisha miaka minne ya chuoni, halafu yapata miaka minne au mitano ya Shule ya Biblia, ndipo mnaweza kutoka nje.”

¹⁶⁰ Lakini Yeye alisema, “Ngojeni katika mji wa Yerusalemu, kwa maana nitawaletea juu yenu ahadi ya Baba. Ndipo mtakuwa mashahidi Wangu,” Luka 24:49, “mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata pande za mwisho za dunia.” Hayo yangali ndiyo matakwa Yake.

¹⁶¹ Mnajua, nimekuwa na ujuzi fulani (nitaharakisha.) na upagani—dini ya kipagani, sanamu. Nimekuwa Afrika, India, nimewaona wale watembeo juu ya moto wanaposimama pale wakiwa na maskini sanamu kubwa mno, yenye macho makubwa, rubi, namna *hiyo*, na rubi kubwa masikioni. Na jinsi hao watu maskini. . . Hao si wanafiki.

¹⁶² Wakulima wanakuja huko nje, nao wanajitayarisha kwa ajili ya jambo hilo, kuhani anawabariki, anawamwagilia maji matakatifu. Na—nao wanachukua ndoana kubwa za samaki

zenye mipira, karibu kubwa *hivi* zilizojaa maji, na kuzichomelea kote mwilini mwao, wakitoa sadaka kwa sanamu. Kisha wanazichukua, wanazichomelea masikioni mwao, wanavishona vinywa vyao pamoja, wanachomelea mkuki humo, kama wamesema uongo, wanashona pua yao na kinywa pamoja, wanaivuta chini. Ndipo basi wanatembea motoni, ukanda wenye upana wa futi nne ama tano, wenye kina cha futi thelathini wakati mwingine, kote kote kwa urefu wa yadi thelathini, kupitia kwenye moto huo, wakijitayarisha kwa ajili ya jambo hilo, kwa ajili ya sanamu.

¹⁶³ Sasa, ibada ya sanamu ni kitu kibaya. Sasa, hebu niliwekee hili msingi kwa muda kidogo tu, maana nitaninii tu. . . matamshi mengine machache, kisha nitafunga. Lakini nataka kufanya hili. Mnaona, ilikuwa. . . Itakuwa kitendawili.

¹⁶⁴ Mpagani, mwabudu sanamu. . . Sasa, Wahindi huku nje, hapa kusini-magharibi, walikuwa wakiabudu sanamu, walikuwa na kile walichokiita mungu wa mvua, alikuwa ni kasa wa matopeni. Walijua aliishi chini kwenye mvua, chini ardhini, nao waliamini ya kwamba huyo mungu wa mvua aliingia kwenye huyo kasa wa matopeni.

¹⁶⁵ Sasa, katika Rumi ya kipagani ya kale walikuwa na Jupita, na wengi wa hao miungu. Nao wanasema ya kwamba miungu hao ni hai, nao walikuwa na vita. Mmesoma visasili, na kadhalika. Kwa hiyo miungu hawa walidhaniwa. . .

¹⁶⁶ Jinsi walivyofanya hilo, walikuwa na madhabahu kubwa mno, nayo sanamu hii ikasimamishwa juu yake, ndipo mwabuduo akaingia, naye akamlipa kuhani kwa ajili ya mshumaa. Nao wakachukua. . . Naye akashuka kwenda hekaluni, wakati mwingine kulikuwako na miungu kadhaa, naye akauweka madhabahuni ili, nadhani, mungu apate kuona njia ya kuiendea sanamu yake sahihi. Nao wakauweka chini pale na kuuwasha mshumaa huu.

¹⁶⁷ Ndipo huyo mwabuduo akaenda na kuchukua. . . Kuhani akaandaa matunda kadhaa, na kutoa dhabihu, kisha akaleta divai, naye kwa kweli alifanya ushirika na hiyo sanamu. Kisha akasajudu mbele ya hiyo sanamu, naye akalala pale katika mzubao mzito sana mpaka huyo mungu wa kuwazia, aliyefanana na ile sanamu aliyokuwa ameitengeneza, akaja na kuingia kwenye sanamu hiyo na kumjibu kupitia sanamu hiyo. Hiyo ni uabudu sanamu.

¹⁶⁸ Huyo mungu wa kuwaziwa, kile walichowazia, kupitia sanamu, kwamba aliweza kumpumbaza mungu huyu kwa dhabihu yake na kwa kuuwasha mshumaa wake, aingie kwenye mungu huyu. Ndipo basi, wakati nafsi yake ilipozongomezwa sana na hayo (Mnaona ambapo ni ibilisi? Mnaona?), naye—naye angewazia ya kwamba mungu alinena tena na dhamira yake kupitia hapo, na kwa kweli ilikuwa ni mungu kwake.

169 Sasa, Mungu alikuwa akitaka kuwaonyesha jinsi Mungu halisi alivyo. Basi kwenye Siku ya Pentekoste, walisujudu siku kumi, wala si la kuwazia, lakini kukaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wenye nguvu ukienda kasi, nao ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi, na Mungu kamwe hakuchukua sanamu, alimchukua mtu aliye hai, na kujiweka Mwenyewe kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu ndani ya mtu huyu, si mungu wa kuwaziwa, si kitu cha kuwaziwa, bali ni uhalisi wa Mungu halisi katika mwanadamu halisi. Ndipo mtu huyu akainuka, na kutenda kazi za Mungu.

170 Ni ajabu kwamba Yeye alifanya hivyo, ajabu kwamba Yeye hakuwachukua watu werevu waliojua jambo fulani kuhusu hilo, wangejaribu kuliwazia, lakini Yeye alichukua kundi la wavuvi wasio na elimu na kuwaweka kule juu. Nao wakasujudu kwa ahadi ya Mungu siku kumi mchana na usiku, ndipo Mungu wa Mbinguni akaja na kukaa ndani ya watu hao.

171 Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Yohana 14:12, Yeye alisema, “Ninii. . . Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya, nyingi kuliko hizi atazifanya, maana Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema katika Marko 16, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ilikuwa ni Mungu aliye hai ndani ya mwanadamu ambaye angeweza kujiweka mbele za Mungu, kulingana na Neno la Mungu, ndipo Neno la Mungu lingedhihirishwa ndani Yake. Amina. Ni—ni kitendawili.

172 Kila unapomwona mtu akiupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni kitendawili. Jinsi Mungu wa Mbinguni anavyojitambulisha katika mtu huyu, akizungumza kupitia kwake, akifanya kazi kupitia kwake, akiishi kupitia kwake, ni kitendawili. Nasi tuko katika sura ya Mungu, naye Mungu alichukua sura Zake Mwenyewe na kujiingiza Mwenyewe katika sura ya sura Yake Mwenyewe alioifanya, kitendawili.

173 Mungu wakati mmoja aliishi ndani ya mwanadamu, halafu dhambi ikamfukuza, ndipo Mungu akamwua Mwanawe Mwenyewe, ndipo akamwacha Mungu arudi na kuishi ndani ya watu Wake tena, naam, bwana. Ni kitendawili. Ni ajabu jinsi anavyofanya jambo hilo.

174 Kanisa, Mungu alilichagua Kanisa Lake liwe ni kitendawili. Jinsi ambavyo alichukua, badala ya wasomi walioadibika, na kuwafanya hao kanisa, hao wanatheolojia, alichukua kundi la wavuvi wasio na elimu, wasio na maarifa. Naye akazitoa funguo za Ufalme, si kwa Kayafa, kuhani mkuu, mwenye elimu. Yeye alifanya nini? Aliwapa wavuvi wasio na elimu, si mtu aliyejua mambo yote ya ndani na nje, Yeye alimpa mtu aliyekuwa amemsujudia Yeye na kumjua. Si, mwajua, si kujua

Kitabu Chake ni Uzima, bali kumjua Yeye ni Uzima. Nazo zile funguo alipewa Petro, kitendawili, kwamba Yeye angefanya hivyo, badala ya Kayafa, mtu mwerevu kuliko wote ka—katika milki ya kidini, Yeye alimpa Petro.

¹⁷⁵ Sasa, mnaamini katika kitendawili? Mzee mmoja mwuza dawa aliniambia si muda mrefu uliopita, akasema, “Ndugu Branham, siku moja wakati wa kuzorota kwa uchumi,” kasema, “mimi na mwanangu tulikuwa tumeketi kwenye duka la dawa,” kisha kasema, “loo, ilikuwa ngumu,” tena kasema, “mwa—mwanamke mjamzito aliingia, alikuwa na maagizo ya kujazwa.” Basi kasema, “Mwanangu alipanda kwenda kumshughulikia, yeye na mumewe.” Kisha kasema, “Alipoangalia yale maagizo,” akasema. . . Mwanamke akasema, ‘Sina pesa za kulipia haya.’ Naye akasema, ‘Pale *pale* ndipo u—ungeninii. . . jimbo lita—litakununulia.’”

¹⁷⁶ Kisha kasema, “Yeye na mumewe wakageuka kwa upole watoke nje, waone kama jimbo lingejaza maagizo hayo.” Kasema, “Kitu fulani kikanigusa, ‘Usimwache mama huyo!’ Kasema, ‘Ni vigumu kwake kusimama kwa miguu yake, sembuse kusimama kwenye mstari ule pale kwa saa kadhaa kusudi maagizo hayo yajazwe.’”

Kasema, “Mwanangu, nenda kamwite, umrudishe hapa.”

¹⁷⁷ Kasema, “Alienda akamwita, na akamrudisha.” Kasema, “Nilirudi pale na kujaza yale maagizo kwa dawa bora sana nilizojua nilikuwa nazo dukani.” Kisha kasema, “Nikaenda nazo, nikazichukua mkononi mwangu, na kuziweka mikononi mwa mwanamke huyo.” Akasema, “Ndugu Branham,” tulikuwa tumeketi tukinywa kimea pamoja, maskini yule mwuza dawa, mtu halisi wa Mungu, akasema, “unajua nini?” Akasema, “Huenda ukafikiri nina kichaa ninaposema jambo hili,” lakini akasema, “nilipoziweka hizo mkononi mwa huyo mwanamke, niliangalia, ilikuwa ni Yesu amesimama pale, nilikuwa nimeziweka mkononi mwa Yesu.” Naam, kitendawili.

¹⁷⁸ Yule Mtakatifu mashuhuri Martin, alikuwa kafiri, baba yake alikuwa, alitaka kumtumikia Mungu. Kulikuwa na sheria huko Ufaransa wakati huo kwamba kama baba alikuwa mwanajeshi, ilimbidi mwanae kutumikia mpaka awe mtu mzima. Sikilizeni kwa makini, basi walipomwita jeshini, alikuwa na mtumishi, na bila shaka, kila askari alikuwa na mtumishi, badala ya huyo mtumishi kumpigia rangi buti zake, alipiga rangi buti za huyo mtumishi. Alikuwa ni mtu mashuhuri, alimpenda Mungu.

¹⁷⁹ Ni kitu gani kilichotukia? Usiku mmoja, usiku wenye baridi wa majira ya baridi kali, pepo zikivuma, watu wakiganda kwa baridi hata kufa kwenye hiyo baridi kali, wakati alipopitia langoni, hapo alilala maskini ombaomba mmoja pale, akisema, “Tafadhalini, mtu anisaidie. Mtu anisaidie. Mtu fulani!” Nao watu ambao wangeweza kumsaidia wakampita.

¹⁸⁰ Martin alikuwa ametoa kila kitu alichokuwa nacho. Naye akaangalia, askari walivaa vazi la begani, koti, alihitaji hilo koti, mwenyewe angeganda, kwa hiyo akavua koti lake, akachukua upanga wake na kulipasua nusu vipande viwili, akamfunika huyo ombaomba kwa kipande chake, akachukua kilichosalia. Watu wakamcheka. “Ni askari anayeonekana wa kuchekesha jinsi gani, amevaa nusu ya vazi la begani!”

¹⁸¹ Lakini usiku huo kwenye kambi ya jeshi, akaamka, na alipoangalia, hapo alisimama Yesu amevikwa kipande hicho cha vazi, hapo walisimama Malaika wamemzunguka pande zote, Naye akawaambia hao Malaika, “Mnajua ni nani aliyenifunika kwa *hili?*” Kasema, “Martin alinifunika kwa *hili.*” Ndipo Martin akajua kile Yesu alichomaanisha aliposema, “Kadiri mnavyomtendea mmojawapo wa watoto Wangu walio wadogo, mmenitendea Mimi.” Wakati alipomfunika maskini huyo ombaomba, alimfunika Yesu, kwa kuwa Yesu alikuwa ndani ya huyo maskini ombaomba, kwa hiyo hatujui ni nani tunayempita. Ilikuwa ni kitendawili. Ninaviamini kwa moyo wangu wote.

¹⁸² Laiti tungejinyenyekeza tu sasa mbele za Mungu, tuamini kwa moyo wetu wote! Hapa wakati fulani uliopita, mtu mashuhuri mwenye elimu alikuja mbele ya kundi la Wapentekoste, alikuwa akitaka kutoa Pentekos-...hotuba ya kiakili na kuwaambia hao watu mahali walipokosea, na yote kuhusu *hili*, na *hili-na-hili*, naye alikuwa nayo yote, hotuba kwelikweli, bali alienda kifua mbele, mwajua, na “*Mimi*, yule jamaa *mkubwa*, mwenye digrii *kadhaa*,” na kadhalika namna hiyo.

¹⁸³ Basi akaanza kuzungumza na Wapentekoste, nao Wapentekoste hawakuipokea. Mnaona? Kwa hiyo akaona alikuwa ameshindwa, kwa hiyo a—akakunja muhtasari wake. Hakuna kitu kilichokuwa kimesemwa kuhusu hiyo hotuba ya kiakili, lakini akijaribu kusema ya kwamba tukio la Kipentekoste la kunena kwa lugha lilikuwa ni uongo, miujiza ya Kipentekoste waliyokuwa wakizungumzia ilikuwa ni ya uongo, hiyo haikuendana na hao watu. Kwa hiyo aliaibika sana hata akachukua kitabu chake cha kiada akaondoka jukwaani.

¹⁸⁴ Kulikuwako na mzee mtakatifu ameketi pale, akasema, “Unajua nini? Kama mtu huyo angalipanda jinsi alivyoshuka, labda angeshuka jinsi alivyopanda.” Kwa hiyo hilo—hilo karibu ni sawa, mnaona. Mnaona, unyenyekevu, kujinyenyekeza mbele za Bwana.

¹⁸⁵ Kwa kweli ni kitendawili. Mungu ni kitendawili. Hayo maono ni kitendawili, kamwe hatuwezi kuyaelezea, jinsi ambavyo Mungu anaweza kuonyesha mambo yaliyokuwako, yaliyopo, na yatakayokuja, ni—ni zaidi ya wowote wa utafiti wetu. Maono ya manabii wa kale, huko nyuma mamia ya

miaka iliyopita, nasi tunayaona bado yakitukia siku hizi, ni kitendawili.

¹⁸⁶ Ilikuwa ni kitendawili, wakati Andrea alipoenda na kumchukua Petro, jina lake lilikuwa Simoni wakati huo, akamleta mbele za Yesu, na kumwambia, kasema, “Mwajua, baba yetu alitwambia kungekuwako na kila namna ya *itikadi* zinazoendelea kabla ya Masihi halisi kuja, bali alitwambia, kulingana na Maandiko, ya kwamba Masihi alipaswa kuwa Nabii, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii, aliye kama mimi.’ Sasa, huyo Masihi atakuwa ni Nabii.” Wayahudi wote wanaamini hilo.

¹⁸⁷ Biblia ilisema, “Akiwepo mtu miongoni mweni aliye wa rohani au nabii, Mimi, Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono, basi yale asemayo yakitimia, basi msikieni.” Sawa.

¹⁸⁸ Kwa hiyo wakati Andrea alipompeleka Petro kule, Naye akamwambia Petro, Yesu alimwambia, na kusema, “Jina lako ni Simoni, na baba yako ni Yona,” Petro alijua papo hapo kwamba hicho kilikuwa ni kitendawili, ya kwamba Mungu alikuwa . . . kabisa Yule wa pekee anayemjua yeye na baba yake mzee angepaswa kuwa ni Mungu.

¹⁸⁹ Wakati Filipo aliposhuka na kumleta Nathanaeli, na kumleta Nathanaeli tena mbele za Yesu, naye akaja Mbele ya Yesu, naye Yesu akasema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake,” hilo lilimshtua.

Akasema, “Ulinijua je, Rabi?”

¹⁹⁰ Sikiza, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Ni macho ya jinsi gani! Maili kumi na tano kuuzunguka huo mlima, Aliona kupitia mlimani, kupitia wakati, na kumwona Filipo chini ya mti.

¹⁹¹ Wakati yule mwanamke kisimani huko Sikari alipokuja kule, kijana mwanamke mrembo, labda kuteka maji. Labda ninii . . . Ilimbidi atoke wakati wanawake wengine waadilifu wameondoka. Yesu alikuwa ameketi pale, mandhari ndogo ya kitu kama *hiki*. Na kwa hiyo, akasema . . .

Akamwambia, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹⁹² Akasema, “Si kawaida, tuna ubaguzi hapa, ninyi Wasamaria, sisi Wayahudi, hatuna uhusiano sisi kwa sisi. Si sawa Kwako kuniuliza, mwa—mwanamke wa Samaria, swali kama hilo.”

Akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema Naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

¹⁹³ Akaendelea, akinena kuhusu kile kisima, jinsi kilivyokuwa kirefu, na yale baba waliyokuwa wamesema, na kadhalika. Nini kilitukia? Katika dakika chache Yeye . . . mwanamke akasema . . . Akaona shida yake, akasema, “Nenda, kamwite mume wako, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

Kasema, “Umesema kweli. Una waume watano, ulikuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

¹⁹⁴ Yeye alisema nini? Sikilizeni, alipofanya hivyo mbele ya Wayahudi, Wayahudi walisema alikuwa akisoma mawazo yao, “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli, ibilisi.” Lakini mwanamke huyu alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua Masihi atakapokuja, Yeye atafanya mambo haya.” Ilikuwa ni kitendawili, mnaona. “Tunajua ya kwamba hapana shaka Wewe ni nabii. Masihi atafanya hivi wakati atakapokuja, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁹⁵ Alijua Huyu alikuwa ni Mungu. Alijua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi, kwa hiyo anaharakisha kuingia mjini na kusema, “Njoni mwone Mtu aliyeniambia ninii. . . shida zangu. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Nao watu wa mji huo wakamwamini Yesu kwa ajili ya neno la yule mwanamke.

¹⁹⁶ Sasa, ninaamini Mungu yeye yule aliyefanya kitendawili wakati huo, anaweza kufanya kitendawili sasa hivi. Mnaamini hilo? Amina. Biblia ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nivumilieni tu kwa dakika moja zaidi.

¹⁹⁷ Kabla hajaondoka ulimwenguni, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sodoma. . . Kumbukeni, uzoa wa Ibrahimu ulikuwa. . . Ibrahimu alikuwa amekuja, akaona mambo haya yote ya Mungu, bali lile ono la mwisho, jambo la mwisho ambalo Ibrahimu aliona kabla tu ya ulimwengu wenye uvuguvugu kuangamizwa. . .

¹⁹⁸ Sasa, kumbukeni, kama ambavyo nimesema sikuzote, kuna matabaka matatu ya watu: asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio. Wote wamethibitishwa, wote walithibitishwa papo hapo: Wasodoma, kama vile ulimwengu siku hizi; mwaminio vuguvugu, huko chini miongoni mwao, wakiishi katika uchafu wao; halafu Ibrahimu, Kanisa teule, lililoitwa na kutengwa.

¹⁹⁹ Malaika alishuka kutoka Mbinguni. Wawili wao walishuka wakaenda kuhubiri Sodoma, hawakufanya miujiza yoyote, waliwapofusha usiku mmoja, kuhubiri Injili kweli humpofusha asiyeamini. Billy Graham mamboleo huko nje miongoni mwa Wasodoma huko nje, akiweka kando. Ninaamini Billy Graham ni mtu wa Mungu, naye huko nje akihubiri ujumbe wake wa toba, na “Tokeni katika Sodoma hii!” Huo ulikuwa ndio ujumbe waliosikia.

²⁰⁰ Lakini kumbukeni, Malaika huyu *mmoja* hakushuka kwenda kule, ila yule Malaika mwingine aliyetumwa kwa Kanisa teule, aliketi, alikuwa mwanadamu, akila nyama,

akinywa maziwa, naye akaketi huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, akamwita Ibrahimu kwa jina lake, ambalo alikuwa tu amepewa na Mungu siku chache kabla ya hapo, naye Sara vivyo hivyo, kasema, “Yu wapi mkeo, Sara?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Akasema, “Nitakuzuru kulingana na muhula wa uhai.”

Ndipo Sara akacheka, akasema, “*Ha!* Mimi, mwanamke mkongwe, nipate raha na bwana wangu?”

²⁰¹ Yeye alisema nini? “Mbona Sara alicheka?” Ndipo Sara akatokea na kujaribu kulikanusha. Ati nini? Alijua alichokuwa akifanya huko nyuma, hilo ndilo jambo lile lile alilofanya Yesu, Alitambua mawazo yao. Kwa nini? Yeye alikuwa ni Neno. Waebrania 4 ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Mtambuzi wa mawazo ya moyo, nia.” Neno, Yesu alikuwa ni Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Sasa, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu. . .” Vipi kuhusu hilo? Je, Mungu alisema uongo? Hawezi kusema uongo, Hawezi kusema uongo, Yeye ni Mungu. Mnaamini hilo? Ninaliamini.

²⁰² Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Mungu na aturehemu. Tulieni kwa dakika moja tu, kitendawili cha kwanza kilikuwa ni wakati ulipookoka, kitendawili kingine kilikuwa ni wakati alipokupa Roho Mtakatifu. Sasa, hebu niwaulizeni jambo fulani. Ikiwa Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. . . Kama niliwaambia roho ya John Dillinger ilikuwa ndani yangu, unatarajia niwe na bunduki, niwe mhalifu. Kama niliwaambia roho ya mchoraji ilikuwa ndani yangu, mngenitarajia, nichukue brashi na kuchora picha, kama ile iliyo ukutani. Na kama nikiwaambia Roho wa Kristo yuko ndani yangu, basi nitafanya kazi za Kristo; hivyo ndivyo alivyosema hasa. Mnaamini hilo? Kama mnaliamini, msilitilie shaka, Mungu atalidhihirisha.

²⁰³ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, nimezungumza kirefu. Nawe ni Mungu. Sasa, jambo pekee ninaloweza kufanya, Baba, ni kunena, Wewe Ndiwe unayepaswa kulidhihirisha na kulifanya kweli. Nami ninakuomba Wewe, Baba, ya kwamba utatujalia majaliwa haya, kupitia Jina la Mwanao, Bwana Yesu, utupe kile tunachotaka, ili watu hawa wapate kujua, hata ukiwa ni mkali, mgumu, unaorarua ndani, hata hivyo umechaguliwa na Wewe, si kwa kijicho, bali kwa upendo ili kuliendeleza Kanisa vema.

²⁰⁴ Biblia ilisema tumepewa kwanza, mitume, manabii, walimu, wachungaji, yote kwa ajili ya ku—kulirekebisha Kanisa, kuliweka Kanisa katika utaratibu. Wakati mwingine wachungaji wetu hutuambia mambo ambayo, yanatuchonga, bali Mungu hulithibitisha kwa mtu aliye na Neno, analithibitisha.

205 Nawe ungali ni Mungu, nami naomba ya kwamba utafanya ijulikane jioni ya leo ya kwamba Wewe ni Mungu, na mambo haya nimeyafanya kwa amri Yako. Mambo haya nimefanya, si kwa nafsi yangu, bali kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa akiniongoza. Ninaomba kwa ajili ya rehema. Ninaomba ya kwamba utatujalia haja za watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo.

206 Sasa, endeleeni tu kuinamisha vichwa vyenu kwa dakika moja na kuomba, iweni na imani. Kama mtaamini, msiwe na shaka! Amini tu kwa moyo wako wote. Aminini ya kwamba Mungu atafanya mambo mengi kwa wingi zaidi, ninaamini Mungu atajitambulisha Mwenyewe.

207 Simjui mtu katika jengo hili nijuavyo mimi, nilimsikia Ndugu Fred Sothmann akisema, “Amina,” nilipokuwa nikihubiri, nje ya huyo, sitahesabu humu jukwaani, maana ninawajua baadhi ya watu hapa, lakini katika kusanyiko. Lakini kama Yesu Kristo, kama yu hai, na amefufuka katika wafu, nanyi watu mna haja huko nje, Yeye yupo hapa kukidhi hiyo. Mnaamini hilo? Endeleeni tu kuomba. “Kama unaweza kuamini!”

208 Sasa, ni wangapi humu ndani ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu, hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa juu. . .? . . . Wengi wenu. Mimi ni mwanadamu kama tu mtu mwingine yeyote. Lakini ninamwamini Yesu Kristo, ninaamini ya kwamba Yeye alifufuka katika wafu, ninaamini ya kwamba Yeye ni Mungu, Yeye ni Mungu ndani yetu sasa katika umbo la Roho Mtakatifu, Naye alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Sasa, kulizungumzia ni jambo moja, bali Kwake kulifanya ni jambo lingine. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

209 Sasa, nakutaka uinue kichwa chako kwa dakika moja tu. Ni wagonjwa wangapi waliomo humu jengoni? Inua mkono wako. Ni watu wangapi walio na mtu mgonjwa ambaye ungeweza kumwombea? Inua mkono wako, mwenye dhambi, chochote kile.

210 Sasa, kulikuwa na maskini mwanamke mmoja wakati mmoja, aliyegusa upindo wa vazi la Yesu na akawa mzima kabisa. Akapitia hapo, na watu wote walikuwa wakimgusa, ndipo—ndipo Yeye akasema. . . Maskini mwanamke huyu akapenya kisiri, akamgusa, akagusa vazi Lake, akageuka na kumwambia. . . Kasema, “Mtu fulani amenigusa.”

211 Ndipo kila mtu. . . Petro akamkemea, “Loo, Wewe unajua jambo kama hilo!” Akasema, “Umati wote unakugusa Wewe. Ungewezaje kufanya. . . ? Ulijuaje ni nani aliyekugusa? Wote wanakugusa. Ati ni nani aliyegu- . . . ?”

212 Lakini akasema, “Lakini naona kwamba nguvu zimenitoka, nimekuwa dhaifu.” Ndipo maskini yule mwanamke aliyemgusa, Yeye aliangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akampata, naye

alipompata, akamwambia shida yake ilikuwa ni nini, nayo imani yake ilikuwa imemponya.

213 Unaamini kwamba Mungu yuyo huyo yu hai? Ingeisaidia imani yako kama angekuja leo na kufanya jambo lile lile? Vipi kuhusu ninyi wafanyabiashara? Mnaamini? Mnaamini? Mtaniombea? Sina hakika na jambo hili, enyi marafiki, sijawahi kuwa na mkutano kama huu miongoni mwa Wafanyabiashara hapa; ninatumaini. Iweni macho, ombeni.

214 Sasa, Neno—Neno, kama nimesema kweli, na kama Mungu akiithibitisha kweli hiyo, Yeye ataonyesha ishara na maajabu, atalionyesha Kibiblia, yale tu Biblia iliyosema. Itabidi iwe ni ishara ya namna hiyo na maajabu. Mnaamini hilo?

215 Kama Yeye angalau...Watu wawili au watatu huko nje kwenye kusanyiko ambao ni wagonjwa, ama wahitaji, ama chochote kile, iwapo tu utaomba. Sasa, angalia, kama utamtazama Mungu na kusema, “Bwana Yesu, Ndugu Branham hanijui, hajui lolote kunihusu mimi, bali ametoa tangazo pale, nimemsikia akilielezea kutoka katika Biblia, ya kwamba Wewe ungali hai, nami nikamsikia akiomba kwamba Wewe ungetuonyesha kitu kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa, kwa hiyo tutaninii... Yule Roho Mtakatifu mkuu tunayeamini tunaye, atajithibitisha Mwenyewe, ya kwamba ni Mungu.” Hiyo ni kweli? Athibitische miongoni mwetu.

216 Sasa, ninyi ombeni, na mwamini tu sasa, na kusema, “Bwana...” Sasa, je, Biblia inasema hivi, enyi wahudumu? Ninyi wahubiri wote mnaoamini jambo hili, angalieni, ya kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu sasa hivi, ameketi mkono wa kuume wa ukuu wa Mungu. Hiyo ni kweli? Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua hilo ni Fundisho la Agano Jipya? Fundisho la Agano Jipya.

217 Vema. Basi huyo Kuhani Mkuu angetendaje, kama ulimgusa Yeye? Kama Yeye ni yule yule, angetenda vile vile, kama yule mwanamke aliyemgusa. Unasema, “Ningalikuwa pale, ningalimgusa.” Vema, unaweza kumgusa sasa hivi, Biblia ilisema hivyo, na hilo ndilo ninaloamini, ni Biblia. Nawe liamini, kwa moyo wako wote, usilitilie shaka.

218 Popote humu jengoni...Sasa, iweni na kicho kabisa. Kwa uchaji tu...Sisemi Mungu atafanya hivyo, sijui. Ni wangapi waliowahi kuiona picha hiyo ya Malaika wa Bwana? Naam, loo, hakika. Tunayo, mnaona. Nilikuwa na hilo katika muhtasari alasiri ya leo, sio wakati wake. Endeeleni tu kuomba.

219 Sasa, Bwana, hii ni...Kama ukitaka, Bwana usiniache nikujaribu. Baba, kamwe sitaki kuwa mtu anayemjaribu Mungu, lakini, Baba Mungu, kama itakutukuza Wewe, basi jalia watu wajue ya kwamba niliwaambia ukweli, nena kwamba nimewaambia ukweli. Tujalie, Bwana. Nilinena habari

Zako vizuri sana nilivyojua, Neno Lako. Hilo ndilo Neno, nilidumu moja kwa moja Nalo, Bwana, haidhuru lilienda wapi, jinsi lilivyo, chochote kile, nilidumu na Neno. Sasa, Baba, ninakuomba Wewe, jibu tena kwamba nimesema kweli, lithibitishe, Baba, katika Jina la Yesu.

²²⁰ Endeeleni tu kuomba, mkisema, “Bwana Yesu, ninaamini hilo, ninaliamini.” Sijui, enyi marafiki, itakuwa ni juu ya Bwana sasa, mnaona. Siwezi kuihisi, kwa namna fulani. Nami ni—niko tu kama maikrofoni hii, bubu kabisa, pasipokuwepo na Kitu fulani cha kuna kupitia kwangu. Mnaona? Lakini hiyo ni karama, njia ya kujituliza Mbele za Mungu, apate kunionyesha, ono. Nilitumaini angefanya hivyo nitakapofika kwenye vitendawili hivyo, lakini labda Yeye hataki kufanya hivyo. Mimi...Kama ndivyo ilivyo, siwezi kulizuiia hilo, mnaona, inanibidi tu kungojea, nione kile Yeye asemacho.

Tulieni kabisa, kila mtu akiomba. Ninaangalia tu kote kwenye wasikilizaji. [Ndugu fulani ananena kwa lugha—Mh.]

²²¹ Sauti ndogo tilivu, iweni na kicho. Vema, unaweza kuinua kichwa chako. Yuko hapa. Sasa ninampa changamoto asiyeamini yeyote, sasa nena la sivyo unyamaze milele. Kama ukiamini tu, omba chochote sasa, mtafute Mungu, uone kama Mungu hatajibu kwamba ni kweli. [Dada mmoja ananena kwa lugha kisha anafasiri—Mh.]

Iweni na kicho kabisa. Ninakutaka, geuza kichwa chako.

²²² Maskini mama anayeketi papa hapa, anaugua ugonjwa wa mkamba kooni mwake. Anatoka Flagstaff. Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile unachoomba. Unaamini, Dada? Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako basi.

²²³ Sasa, hebu nirudie maombi yake, alikuwa akisema, “Bwana, ninateseka *sana*, jalia Ndugu Branham anene nami.” Punga mkono wako kama vitu hivyo...kama ulikuwa ukiomba ili—ili nikuite wakati huo? Nilipokuita, ulikuwa ukiombea hilo, hiyo ni kweli? Punga mkono wako namna *hii*, ni kweli. Hivi hatufahamiani? Punga mkono wako tena. Sikujui. Endapo hiyo ni kweli, punga mkono wako tena. Vema. Aligusa nini?

²²⁴ Kuna mama aliyeketi papa hapa nje ambaye anamwombea rafiki aliye na kansa. Unaamini kwa moyo wako wote? Mungu atayajibu maombi yako. Kumwona mtu, mwanamume, mgonjwa sana, sana. Kama utaamini kwa moyo wako wote (ninaangalia ono.), Mungu akubariki, unaweza kulipata.

²²⁵ Simjui huyo mwanamke, sijawahi kumwona. Kama hiyo ni kweli...Mama huyu aliyeketi moja kwa moja hapa, ninamwangalia, haya basi. Si ulikuwa umeketi pale ukiomba, “Bwana Yesu, jalia hili...”? Mungu akubariki.

Mtu fulani aombe.

226 Hapa—huyu hapa m—mtu ameketi mumu humu ndani. Hivi hamwioni hiyo Nuru? Moja kwa moja juu ya maskini mwanamke mwenye mvi aliyeketi papa hapa chini? Naam, huyo mama aliyeinua mkono wake. Ana kisukari. Yeye si mwenyeji wa hapa, ametoka nchi yenye milima, Uswisi. Kuna kundi zima lenu hapo kutoka Uswisi. Hiyo ni kweli. Amini, nawe unaweza kurudi nyumbani, uwe mzima.

Unaamini?

227 Huku nyuma, ninyi watu, hapa, huyu hapa mama ameketi papa hapa. Sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini anaugua ugonjwa wa koo lake, ugonjwa wa macho yake, ameketi papa hapa akiniangalia. Yeye ni mhubiri mwanamke. Simama kwa miguu yako na ukubali, mama. Uwe mzima.

Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hebu jaribu kuficha dhambi yako sasa.

228 Huyu hapa mwanamume. Amekuwa akitoa maoni yake kunihusu. Hiyo ni kweli, bwana. Kazi yako ni mwalimu, nawe una matatizo ya kiroho usiyoyaelewa. Kama ndivyo ilivyo, inua mkono wako. Yote yatatatuliwa. Unikubali mimi kama nabii wa Mungu, ninakwambia kweli, BWANA ASEMA HIVI.

Unaamini?

229 Huyu hapa mama aliyeketi papa hapa nyuma. Anaugua ugonjwa kwenye titi lake, amefanyiwa upasuaji mara tatu. Anaukosa. Jalia. . . Mungu anisaidie. Binti Alexandra, pokea uponyaji wako katika Jina la Bwana Yesu. Kama hilo ndilo jina lako, na hilo. . . hatufahamiani, simama kwa miguu yako, simama kwa miguu yako, kama hiyo ni kweli.


230 Sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Unaamini hilo? Kama huyo si Yesu yeye yule aliyeishi wakati mmoja! Sijui, mimi ni mwanadamu. Unaamini? Mpokee.

231 Hapa, kuna mwanamke aliyeketi papa hapa chini, simjui, sijawahi kumwona. Yeye ni nesi, naye anamwomba mgonjwa wake. Mgonjwa anaugua ugonjwa wa akili. Hatufahamiani, sivyo? Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, itakusaidia? Itawasaidia wasikilizaji? Huu hapa mkono wangu, sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Ikiwa hatufahamiani, inua mikono yako, mama. Wewe ni Bibi Brandon. BWANA ASEMA HIVI!

232 Mnaamini, ninyi nyote (Hicho ni kitendawili? Mbona, Yeye angali ni Mungu!), kwamba Roho Mtakatifu yuko kila mahali hapa sasa? Mnaamini hilo? Sasa, Maneno ambayo nimesema ni ya kweli, Mungu amelithibitisha.

233 Sasa, unamwamini Mungu kwa moyo wako wote? Basi wekeaneni mikono, anzeni kuomba mpate ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mngewezaje kuwa karibu zaidi na Yesu Kristo kuliko mlivyo sasa hivi? Wekeaneni mikono na kuomba jinsi

mfanyavyo katika kanisa lenu wenyewe, kwamba Mungu atawajaza kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, nanyi mtaona kitendawili msichowahi kuona hapo kabla. Aminini! Mungu atawaonyesha kitendawili halisi.

²³⁴ Ee, Bwana Mungu, yasikie maombi haya ya mtumishi Wako, na jalia ibilisi aliachilie kusanyiko hili sasa hivi, kupitia nguvu na kufufuka kwa Yesu Kristo. Amina. 

62-0128A Kitendawili
Ramada Inn
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org